# Nipashe

Jumatano Mei 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580942

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,255,316,060

BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Bunge** laagiza mapitio vigezo mikopo ya elimu

UKURASA 4



**HAALAND KUTHIBITISHWA RASMI MAN CITY WIKI HII**

UKURASA 21



# UAMUZI MGUMU

• **Serikali** yaingiza bilioni 100/- kunusuru makali mafuta, Museveni ampa Samia mbinu kudhibiti... *Endelea ukurasa 2*





Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika mazungumzo na mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Uganda, Yoweri Museveni, katika Ikulu ya Entebbe, Uganda jana. **PICHA: IKULU**

## Mgogoro wa KKKT Konde wahamishiwa mahakamani

UKURASA 3



## Neema tele sekta ya elimu 2022/23

UKURASA 3


**MICHEZO** NABI AMTETEA MAYELE PENALTI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper (wapili kulia), akikabidhi kompyuta kwa walimu wa sekondari na shule za msingi, Wilaya ya Babati mkoani Manyara juzi. Benki hiyo, imekabidhi kompyuta 25 na mabati 200 kwa shule mbalimbali wilayani humo. Watatu kulia ni Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, Paulina Gekul. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yachukua uamuzi mgumu kupunguza bei mafuta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imechukua uamuzi mgumu wa kupunguza bei ya mafuta nchini kwa kutoa ruzuku ya Sh. bilioni 100 na ahueni hiyo itaanza Juni Mosi, mwaka huu.

Nafuu nyingine ya bei ya mafuta itatokana na mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ambayo itapatikana katika mwaka ujao wa fedha ambayo pia itatoa ahueni kwenye kupanda kwa bei za bidhaa.

Sambamba na hayo, serikali imetaja hatua saba zisizo za kifedha zilizochukuliwa ikiwamo kuruhusu watu wenye uwezo wa kuingiza mafuta kwa bei nafuu.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alitangaza hatua hiyo jana bungeni alipokuwa akitoa taarifa ya serikali kuhusu suala hilo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Bunge lililotolewa wiki iliyopita.Alisema ruzuku hiyo inatolewa kwa kupunguza matumizi ya serikali katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha 2021/22 na haitagusa miradi ya maendeleo ambayo inaendelea.

"Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, amaelekeza kwamba mwaka ujao wa fedha ni mbali. Ahueni itafutwe mapema zaidi, hivyo kama hatua ya dharura, Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwamba katika kipindi hiki kabla hatujafikia mwaka mpya wa fedha, serikali ijibane na ijinyime ili zitolewe Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza bei za mafuta nchini.

"Ruzuku hii itatolewa kwa ajili ya kupunguza bei kuanzia Juni 2022. Hii ni kutokana na kuwa wafanyabiashara wa jumla wamekwishalipia gharama ya mafuta ambayo imejumuishwa katika bei hizi za Mei 2022 na wafanyabiashara wa mafuta katika vituo wamekwishanunua mafuta kwa bei hii inayotumika sasa,"alisema.

### NAFUU NYINGINE

Waziri Makamba alisema mchakato wa kuchukua mkopo kutoka IMF na Benki ya Dunia uko mbioni kukamilika na ahueni kwenye kupanda kwa bei za bidhaa itapatikana katika mwaka ujao wa fedha.

"Nafuu nyingine inayotokana na mikopo itakuja katika mwaka ujao wa fedha itaelezwa kwa kina zaidi na Waziri wa Fedha kwenye bajeti ya serikali mwezi ujao," alisema.

Hata hivyo, alisema Tanzania inayo mafuta yanayotosheleza na ziada kwa kiwango kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria na itaendelea kuchukua hatua madhubuti ili kusitokee upungufu.

"Sheria inataka nchi iwe na mafuta ya ziada kwa siku 15 lakini kwa Tanzania mafuta ya petroli yapo kwa siku 34 wakati mafuta ya dizeli yapo kwa ziada ya siku 34, mafuta ya taa siku 38 na mafuta ya ndege kuna ziada kwa siku 28,"alisema.

Waziri Makamba alisema kupanda kwa mafuta ni janga kubwa kwa nchi lakini ni hatari kubwa kwa usalama wa nchi yoyote, hivyo Tanzania itaendelea kuwa makini kwenye jambo hilo lisilete madhara.

"Kwa sasa serikali inaendelea na mkakati wa namna ya kupunguza makali ya bei ya mafuta kwa kutenga Sh. bilioni 100 kwenye mpango wa muda mfupi na muda mrefu gharama zake zitatajwa na Waziri wa Fedha na Mipango kwenye bajeti ya serikali," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na hali ilivyo duniani yakiwamo majanga ya vita, bei ya mafuta itaendelea kupanda katika soko za dunia, hivyo kuendelea kuathiri nchi nyingi ikiwamo Tanzania ambayo haina visima vya mafuta.

### HATUA SABA

Alisema Wizara imekamilisha kufanya tathmini ya kampuni zote zilizoonyesha nia ya kuagiza mafuta kwa bei nafuu kwa lengo la kujiridhisha na uwezo wao wa kuleta bidhaa hiyo ili kuhakikisha uwapo wa mafuta nchini kutokana na hali hiyo, alisema inatarajiwa bei za mafuta zitapungua zaidi kuanzia Agosti, mwaka huu.

"Hatua ya pili ni Kuanzisha Mfuko wa Kuhimili Ukali wa Bei za Mafuta (Fuel Price Stabilization Fund). Serikali imeandaa utaratibu wa kuanzisha mfuko maalumu utakaotumika kupunguza makali ya bei ya mafuta kipindi ambacho bei hizo zinaongezeka kwa kiasi kikubwa,"alisema.

Alibainsiha kuwa mpango wa kuanzisha mfuko huo upo katika hatua za mwisho za maandalizi na utakapokamilika, utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri.

"Hatua ya tatu ni Kuanzisha Hifadhi ya Mafuta ya Kimkakati (National Strategic Petroleum Reserve). Serikali inakamilisha marekebisho ya kanuni za kuanzisha na kuendesha hifadhi mafuta ya kimkakati ili nchi yetu ijihakikishie usalama wa upatikanaji wa mafuta na unafuu wa bei katika vipindi kama hivi,"alisema.

Wairi aliitaja hatua ya nne ni kuwa na kituo kikubwa cha mafuta (Petroleum Hub) na kwamba serikali inakamilisha makubaliano ya kujenga maghala makubwa ya kuhifadhi mafuta kwa ajili ya kuuzwa ndani na nje ya nchi kulingana na uhitaji,"alisema. Makamba alisema uwapo wa kituo hicho utasaidia nchi kupata mafuta yenye bei nafuu pale bei zinapopanda kupita kiasi na mpango huo utekelezaji wake utakamilika katika kipindi cha miaka mitatu.

"Hatua nyingine ni kuanzisha upokeaji wa mafuta katika ghala moja (Single Receiving Terminal - SRT) kupitia maghala ya TIPER ili kupunguza au kuondoa gharama za meli kusubiri au kuchukua muda mrefu katika upakuaji wa mafuta katika maghala mengi. Gharama hizi nazo zina mchango katika bei ya mafuta,"alisema.

Hatua hiyo, alisema itaondoa tatizo la udanganyifu na kuongeza ufanisi katika biashara ya mafuta hapa nchini.

"Hatua hii inaendana na kuyafanya maghala haya kuwa 'customs bonded warehouse' ili kushamirisha biashara ya mafuta yanayokuja nchini na kwenda kwenye nchi nyingine,"alisema.

Alizitaja hatua nyingine ni kuliongezea uwezo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuagiza mafuta nje ya nchi ambapo kwa mara ya mwisho ilifanya shughuli hiyo miaka 20 iliyopita.

"Hatua nyingine ni kuimarisha utendaji na weledi wa taasisi za serikali zinazoshughulika na biashara ya mafuta nchini, ikiwamo EWURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji) na PBPA (Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja).

# Museveni ampa Samia mbinu bei ya mafuta

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema amejifunza njia nzuri za kupambana na ongezeko la bei za mafuta kutoka kwa Rais Yoweri Museveni wa Uganda na atazitumia akiwa nchini ili kukabiliana na tatizo hilo.

Aliyasema hayo jana Uganda katika hafla ya kutia saini hati za makubaliano ya mkataba katika wizara za ulinzi na nishati za Tanzania na Uganda ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kiserikali ya siku mbili nchini humo iliyoanza jana.

"Tulikuwa tunajadili kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta na akanipa mikakati mizuri ya kuiangalia na ninafikiri nitakwenda kuitumia nchini kwangu ili wote tuwe na njia bora za kupambana na kupaa kwa bei ya mafuta," Rais Samia alisema.

Aliongeza kuwa nchi hizo mbili zimeamua kuweka msukumo katika ushirikiano wa biashara na uwekezaji na moja ya mikakati wanayoijadili ni kuondoa vikwazo visivyokuwa vya kiforodha.

"Kwa mantiki hiyo, ninatumia nafasi hii kuwakaribisha wananchi wa Uganda nchini Tanzania ili kukuza biashara na uwekezaji, kuna nafasi chungu nzima zinawasubiri," alisema Rais Samia.

Alizitika wizara zilizotia saini makubaliano hayo kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa haraka ili kuvuna matunda yake ndani ya muda mfupi.

Alisema nchi hizo mbili kama zilivyo zingine, zinapitia athari za mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vya Russia na Ukraine, hivyo juhudi za pamoja zinahitajika katika kuzikabili.

"Na sasa tunapitia changamoto zinazotokana na vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vinahitaji nguvu ya pamoja kuzikabili ili kuimarisha uchumi, ndiyo maana nilipopata mwaliko kutoka kwa Rais Museveni, sikufikiria mara mbili kuukubali," alisema Rais Samia.

Alieleza kuwa nchi hizo majirani zinapitia kero zinazofanana, hivyo zinahitaji ushirikiano wa karibu kubadilishana mawazo ya jinsi ya kuzihudumia nchi zao vizuri.

"Kwa mantiki hiyo, nipo hapa kuboresha uhusiano wetu huku nikitafuta njia nzuri za kuboresha ushirikiano wetu," Rais Samia alifafanua.

Alisema kabla ya halfa hiyo walifanya mazungumzo na Rais Museveni yaliyoangazia mambo mbalimbali ikiwamo uchumi, amani na usalama, miundombinu na elimu.

"Tumeridhishwa na utulivu wa kisiasa ambao nchi zetu zinafurahia, kwa upande mwingine tumejadili namna tutakavyofanya kazi pamoja kudumisha amani na usalama katika nchi zetu ili ushirikiano wa Afrika Mashariki uendelee kuwa imara," alisema Rais.

Mwenyeji wake Rais Museveni alisema uhusiano baina ya nchi hizo mbili unaendelea kudumu ndiyo maana wanatekeleza miradi ya kimkakati ikiwamo usafirishaji, nishati, uhusiano wa mambo ya nje na ulinzi na usalama.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, alisema ziara hiyo ni ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kijamii na kiuchumi.

# Neema tele sekta ya elimu

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

NI neema! Ndivyo ambavyo yeyote anaweza kusema kutokana na mikakati ya serikali katika sekta ya elimu kwa mwaka ujao wa fedha.

Imesema kuwa kufikia mwishoni mwa mwaka huu itafanya uamuzi ulioainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 22014, ikiwamo utekelezaji wa utoaji wa elimu ya msingi kwa miaka 10 badala ya saba ya sasa.

Imesisitiza kuwa ifikapo Desemba mwaka huu, uchambuzi utakuwa umekafanyika na kukamilika kuhusu sera hiyo ili uamuzi ufanyike kuhusu utekelezaji.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/23, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.49.

Prof. Mkenda alisema kazi kubwa itakayofanyika katika mwaka wa fedha wa 2022/23 itakuwa ni mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa minajili ya kufanya uamuzi kuhusu mambo kadhaa ambayo sera imeainisha lakini hayajatekelezwa.

“Kwa mfano, sera inaainisha kwamba elimu ya lazima itakuwa ni ya miaka 10, lakini bado tunatoa elimu ya lazima ya miaka saba.

“Tunatarajia kuwa kabla ya mwisho wa mwaka huu uchambuzi utakuwa umefanyika na kukamilika kuhusu sera hii ili uamuzi ufanyike kufanyika kuhusu utekelezaji,” alisema Prof. Mkenda.

Alieleza kuwa pamoja na uchambuzi huo, juhudi zitaendelea za kukusanya maoni ya wadau wote ili uamuzi utakapofanyika uzingatie maoni ya wadau wote na uchambuzi wa kitaalamu. Prof. Mkenda alisema mapitio ya sera hiyo yatatoa dira ya mabadiliko yatakayohitajika katika Sheria ya Elimu ya mwaka 1978.

“Tunatarajia pia kuwa ifikapo Desemba mwaka huu wizara itakuwa imekamilisha rasimu ya mabadiliko ya mitaala itakayozingatia maoni ya wadau na mwelekeo wa Sera ya Elimu utakaokuwa umependekezwa,” alisema Prof. Mkenda.

**MAENEO YA MKAKATI**

Prof. Mkenda alisema kwa mwaka 2022/23 wizara yake itajikita katika maeneo ya mkakati ikiwamo kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi nchini.

Alisema eneo lingine ni kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini.

Prof. Mkenda alisema pia watajikita katika kuongeza wigo wa shule za ufundi za elimumsingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea vijana stadi na maarifa yanayohitajika katika soko la ajira.

Eneo lingine ni kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za elimu ya juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenye kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali nchini.

Alisema pia watajielekeza katika kutekeleza juhudi za kukuza sayansi nchini kwa kutoa ufadhili wa asilimia 100 wa kulipia gharama za masomo za chuo kikuu wanafunzi watakaoongoza katika mitihani ya masomo ya sayansi ya kidato cha sita.

Prof. Mkenda alisema pia kwa Watanzania watakaofanya vizuri kwenye masomo yao ya vyuo vikuu kwenye nyanja za sayansi, teknolojia na tiba ili kusoma kwenye vyuo vilivyo bora zaidi duniani.

Alisema watajielekeza katika kuhimiza utafiti wa kisayansi na tiba kwenye vyuo vikuu kwa kutoa tuzo ya Sh. milioni 50 kwa mhadhiri yeyote atakayeweza kuchapisha matokeo ya utafiti wake kwenye majarida yenye hadhi ya juu kabisa ya sayansi na ya elimu ya tiba.

Prof. Mkenda alisema watajielekeza katika kuhamasisha sekta binafsi na wadau mbalimbali kufadhili Watanzania kwenda kusoma kwenye vyuo bora duniani.

***Soma hotuba ya Prof. Mkenda Uk. 11 hadi 15**

# Mgogoro wa KKKT Konde wahamishiwa mahakamani

**Na Waandishi Wetu,**
MBEYA

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde umechukua sura mpya baada ya Askofu wa Dayosisi hiyo aliyeondolewa madarakani, Dk. Edward Mwaikali, kukimbilia mahakamani na kufungua kesi ya kupinga kuondolewa kwake.

Mgogoro huo ambao umedumu kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, ulisababishwa na kuhamishwa kwa Makao Makuu ya Dayosisi hiyo kutoka Tukuyu wilayani Rungwe kwenda jijini Mbeya na kusababisha pande mbili kuanza kusigana.

Katika harakati za kuumaliza mgogoro huo, Mkuu wa Kanisa la KKKT, Askofu Dk. Fredrick Shoo, aliitisha mkutano mkuu wa dharura wa dayosisi hiyo Machi 22, mwaka huu, ambao ulitumika kumwondoa Askofu Mwaikali madarakani na kumchagua Mchungaji Geofrey Mwakihaba kuwa Askofu wa Dayosisi hiyo.

Hata hivyo, Dk. Mwaikali na wafuasi wake walipinga uamuzi huo wakidai kuwa mkutano ulioitishwa na Askofu Shoo ulikuwa batili, kwamba ulikiuka Katiba ya Dayosisi hiyo na hivyo wakawa hawamtambui askofu mteule.

Vilevile, walikuwa wanapinga uamuzi huo wakidai kuwa wakati wa usuluhishi wa mgogoro huo, upande wa Askofu Mwaikali haukushirikishwa na hivyo wanamtuhumu Askofu Shoo kuwa alisikiliza upande mmoja.

Kutokana na mgogoro huo kuendelea kurindima, hivi karibuni Askofu Mwaikali pamoja na wafuasi wake waliamua kukimbilia katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya ambako walifungua kesi ya kupinga kuvuliwa madaraka.

Kwa mujibu wa Wakili wa Upande wa Mashtaka, William Mashoke, ni kwamba washtakiwa katika kesi hiyo namba 14 ya mwaka 2022 wapo 30 ambao ni pamoja na Bodi ya Wadhamini wa KKKT, Mkuu wa KKKT, Dk. Shoo, aliyekuwa Katibu wa Mkutano Mkuu wa dharura, Jackson Mwakibasi.

Wengine ni Askofu Mteule wa Dayosisi hiyo, Geofrey Mwakihaba, Msaidizi wa Askofu Mteule, Dk. Meshack Njinga na watu wengine 24 ambao walishiriki kwenye Mkutano Mkuu wa dharura uliomwondoa Dk. Mwaikali madarakani.

Wakili Mashoke alidai kesi hiyo ilianza kusikilizwa jana chini ya Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, James Karajemaha ambapo washtakiwa wote hawakufika mahakamani licha ya kupatiwa wito na mahakama hiyo.

“Lakini kesi hii imeahirishwa ili kutoa nafasi kwa pande hizi mbili kupatana nje ya mahakama na kuwapelekea taarifa ya wito washtakiwa na kesi hii imepanga kusikiliza tena kesi hii Mei 18 mwaka huu,” alidai Wakili Mashoke.


EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UOKOZI NA MATIBABU, TANZANIA
## KUMBUKUMBU NO: 10007711

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), kampuni ya mafuta na gesi, inaalika mashirika yenye uzoefu na yanayoheshimika kuonesha nia ya kutoa huduma za uokozi na matibabu kwa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 296 ziko Uganda na 1,147 ziko Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

**Mawanda ya kazi/utaratibu wa program ya kutoa huduma ya uokozi na matibabu**

1. Kutathimini miundombinu ya afya kwenye mkuza wa bomba la mafuta na na njia za usafirishaji mtoa huduma atatakiwa kufanya ukaguzi halali na wa uhakika kwa kila sehemu (site) ambao utatathimini juu ya uwezo wa miundo mbinu.
2. Kufanya tathmini ya ndege iliyopo ya uokoaji itakayotumika wakati wa uokozi. Kupitia na kutathmini watoa huduma za kusafirisha na muda wa uokozi wa ndani ya nchi na nje ya nchi, ikihusisha na tathmini ya mpango na manajiment ya barabara za ndani, na uwezo wa uokozi kwa njia ya anga kwenye bomba la mafuta.
3. Uundaji wa suluhisho mahususi la Usaidizi wa Kimatibabu ambalo litamwezesha Mtoa Huduma kuunga mkono uratibu wa Huduma za Uokoaji wa Matibabu kulingana na utaratibu wa kawaida wa kufanya kazi, ikijumuisha uundaji wa mpango wa Mradi wa uokoaji wa matibabu (MEDEVAC).
4. Mawanda ya hiari-Utekelezaji na usimamizi wa vituo vya matibabu kwenye maeneo yote ya kazi za mradi:

- Utoaji wa usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi wa Matibabu
- Usimamizi wa Vifaa vya Matibabu vya Mkandarasi kwenye Maeneo husika
- Wafanyakazi na kuendesha klininiki za wakandarasi
- Utoaji wa huduma za usimamizi wa ubora wa matibabu
- Utoaji wa huduma za afya kazini
- Huduma za Kinga na afya ya umma
- Utoaji na ushauri, ukaguzi na uwezo wa utaalam
- Huduma za afya ya jamii
- Utoaji wa matibabu kwa njia ya teknolojia ya mawasiliano.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni inayotaka kuonyesha nia yanatakiwa kuwa na vielelezo vifuatavyo:

- Leseni ya Biashara.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) na cheti kinachoonyesha uthibitisho ulipaji wa kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) au uthibitisho wa maombi ya kusajiliwa wakati wa kuwasilisha nia yake ni muhimu sana.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani
- Uzoefu wa wa utoaji wa huduma ya uokozi na matibabu kwenye miradi inayofanana na mradi wa EACOP katika ukubwa, mawanda na kijiografia.
- Umahiri na uwezo katika kutoa Huduma za Uokoaji wa Matibabu kama ilivyoainishwa hapo juu kwa kiwango kikubwa, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa, na kwa uzoefu wa angalau miaka 10/utendaji wa huduma kama hizo.
- Wafanyakazi waliohitimu na wenye uzoefu katika kutoka huduma za Uokoaji/uokozi na matibabu kwa miradi ya mafuta na gesi ambayo inatii mahitaji ya IFC.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za muda wa miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, Usalama mahala pa kazi na Mazingira (QHSE), taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani ya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa kupambana na rushwa na sera za ufuatiliaji
- Uthibitisho wa leseni unaofaa kutoka kwa mamalka husika ndani ya nchi kwa ajili ya huduma

Makampuni yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** saa au kabla ya saa **10 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **27th May 2022.** Ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb.** Taarifa zote ziwasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho. Taasisi zitakazokidhi vigezo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, akizungumza wakati akifungua kikao cha Baraza Kuu la Chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bunge lataka mapitio ya vigezo mikopo wanafunzi elimu ya juu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limeiagiza serikali kuangalia upya vigezo vya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ili kupunguza malalamiko kutoka kwa wadau wakiwamo waombaji na wazazi.

Pia limeiagiza serikali kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) inaanza kujiendesha kibenki, ili kuwezesha na kurahisisha utoaji na ukusanyaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaohitaji mikopo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Aloyce Kamamba, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo wa kamati kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2022/23.

Kamamba alisema serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuwapatia mikopo wanafunzi wa elimu ya kati pamoja na kuangalia upya vigezo vya utoaji wa mikopo ili kupunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu, yanayojitokeza mara kwa mara.

"Serikali iendelee kutafuta vyanzo vya fedha ili kuwapatia mikopo wanafunzi wote wanaohitaji mikopo. Bodi ya mikopo ijiendeshe kibenki ili kuwezesha na kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaohitaji mikopo," alisema.

Kuhusu upungufu wa watumishi katika taasisi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwamo uhaba wa walimu na wakufunzi, Kamamba alisema wizara inapaswa kuwa na mkakati wa dhati wa kutatua kero hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watumishi ili kukidhi mahitaji.

Alisema serikali pia iendelee kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari, pamoja na vyuo vikuu viendelee kuwa na uhuru wa kitaaluma katika kuajiri watumishi wake hususani wanataaluma kwa kuzingatia sheria kanuni na vigezo vya kitaaluma.

Kuhusu madawati ya jinsia shuleni na vyuoni, Kamamba alisema yanapaswa kuanzishwa ili kuwezesha vijana kupata elimu ya afya ya akili, namna ya kukabili athari za unyanyasaji wanaokumbana nao ukiwamo unyanyasaji wa kingono.

Pia, alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ihamasishe wazazi kuongea na vijana wao kuhusu hatua za mabadiliko ya mwili na elimu ya afya ya uzazi.

Alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapaswa kuwekeza katika kutoa mafunzo ya elimu ya afya ya uzazi kwa walimu, ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu hiyo na wanakuwa na maadili.

## NOTISI/TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | RWEZAULA ASELY VICENT | GARI TOYOTA ALPHARD T632 DFF | WILLIAMS HUBERTS MTENDAMEMA | MAGOMENI MIKUMI | 25/05/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | CEFI GENERAL TRADERS | NYUMBA | ERNEST FELIX IGANGA | BUGARIKA-MWANZA | 25/05/2022 SAA NNE ASUBUH NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0628338064/0689349477
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## Mkumbo: Itachukua miaka 18 kumaliza tatizo ajira za walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo, amesema itachukua angalau miaka 18 kumaliza uhaba wa walimu ikiwa serikali itaendelea na kasi yake ya kuajiri walimu 10,000 badala ya 20,000 hadi 30,000 kwa mwaka.

Ili kumaliza tatizo hilo, amesema serikali inatakiwa kuajiri walimu 116,427 kwa mwaka kuanzia mwakani ili kuendana sambamba na idadi ya wanafunzi itakayokuwapo ifikapo mwaka 2026.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2022/23, alisema mahitaji ya walimu nchini ni 433,992 (274,549 wa shule za msingi na 159,443 wa sekondari).

Prof. Mkumbo alisema walimu waliopo ni 258,291 (173,591 wa shule za msingi na 84,700 wa shule za sekondari).

"Tuna upungufu wa walimu 175,701, sawa na asilimia 40.5. Kwa kasi ya sasa ya kuajiri walimu 10,000 kwa mwaka, tutahitaji miaka 18 kuziba pengo lililopo," alisema na kubainisha kwamba tatizo kubwa liko zaidi kwa upande wa masomo ya sayansi na hisabati.

"Kwa mfano, kati ya walimu 70,327 wanaohitajika kwa masomo ya sayansi na hisabati kwa shule za sekondari, waliopo ni walimu 23,647 pekee, sawa na asilimia 33.62, Kuna imani kwamba upungufu wa walimu ni vijijini pekee. Si kweli. Dar es Salaam, kwa mfano, kati ya walimu 3,894 wanaohitajika kwa masomo ya sayansi na hisabati, waliopo ni 1,298 pekee.

"Upungufu wa walimu wa sayansi na hisabati ni asilimia 66.38 ni takribani theluthi mbili. Huwezi kujenga uchumi wa viwanda bila sayansi, hesabu na teknolojia, lazima tuwekeze katika kufundisha walimu wa hesabu na teknolojia," alisema.

Prof. Mkumbo alisema inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2026 kutakuwa na wanafunzi wa elimu ya awali, msingi, na sekondari milioni 23.6, hivyo kunahitajika walimu 724,000 ifikapo mwaka 2026.

"Hii inamaanisha kuwa tutahitaji kuajiri walimu 116,427 kila mwaka kuanzia mwakani. Napendekeza muda wa mafunzo ya ualimu katika vyuo vikuu urudi kuwa miaka minne. Mwaka wa nne wote wanafunzi watumie katika mafunzo ya vitendo shuleni. Hivyo kwa kila mwaka tutakuwa na uhakika wa walimu zaidi ya 15,000 wanaingia shuleni," alisema.

Katika kupunguza nafasi za utawala katika elimu, Prof. Mkumbo alishauri ifutwe kada ya maofisa elimu kata na kuimarisha nafasi za wakuu wa shule.

"Aidha, ofisa elimu wilaya awe moja na ajikite katika kuhangaika na miundombinu ya elimu. Masuala yote yanayohusu taaluma na walimu yashughulikiwe na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC),"alisema.

Pia alisema serikali irudishe posho za kufundisha iliyokuwa inalipwa kwa walimu na kupendekeza ilipwe kwa walimu wa sayansi, hesabu na lugha ambayo ni Sh. 4,000 kwa siku na kwa mwezi Sh. 100,000.

**HABARI KIMATAIFA**

## Ekari 500 mpunga zavamiwa na ndege

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

ZAIDI ya ekari 530 za mpunga katika kata za Mbigiri, Tindiga na Kilangali, Kilosa mkoani Morogoro zimeshambuliwa na ndege wasumbufu aina ya kweleakwelea na kuwaacha wakulima kubaki na taharuki ya kukumbana na baa la njaa.

Jaffari Mpoto, mmoja wa wakulima katika eneo hilo, alisema zaidi ya wiki moja imepita tangu kuvamiwa na ndege hao ambapo wanalazimika kutumia saa 12 shambani kulinda mazao yao.

Alisema hali imekuwa mbaya zaidi kwa sababu wamelazimika kuacha shughuli zingine za maendeleo na kuhamia shambani ambako imewalazimu watu wawili au zaidi kulinda shamba la ekari moja.

"Yaani sasa hivi tukitumia mbinu za kienyeji kupiga ngoma na mayowe ili kufukuza ndege hawa tena tunawahi kufika saa 12 asubuhi na kuondoka saa 12 jioni. Sasa unakuta mtu una zaidi ya ekari 10 na ndege walivyo wengi ekari moja inabidi uweke vibarua watatu au wane," alisema Mpoto.

Kutokana na janga hilo, Diwani wa Kilagali, Amos Kusupa, aliiomba serikali kufanya jitihada za haraka kukabiliana na ndege hao kwa sababu asilimia kubwa ya wakulima katika maeneo hayo hutegemea mazao hayo kwa chakula.

Alisema nguvu za wananchi kukabiliana na ndege hao haziwezi kuzaa matunda kwa sababu njia wanayotumia ni ya kienyeji kwa kupiga ngoma au kelele jambo ambalo haijazaa matunda hadi sasa na mazao yanaendelea kuteketea.

"Njia wnayotumia wananchi ni ya kuzamani sana hasa ukilinganisha na idadi ya ndege waliovamia ndiyo maana unaona ndani ya wiki moja kila mkulima amechoka na wengi wao wanategemea kilimo hiki kwa chakula na biashara," alisema Kusupa.

Ofisa Mdhibiti Visumbufu Wilaya ya Kilosa, Mayowela Hasanali, alisema baada ya kupata taarifa ya uwapo wa ndege hao waharibifu, hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ikiwamo utafiti wa kubaini makazi ya ndege hao katika sehemu tatu.

# Tanzania ya kwanza Afrika matumizi nyenzo tathmini

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imependekezwa na Sekretarieti ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika kufanyiwa majaribio ya matumizi ya nyenzo ya tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Maadili na Misingi ya Utumishi wa Umma na Utawala ambayo itakuwa ikitumika kuzitathmini nchi wanachama.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akifungua semina ya kuwajengea uwezo wataalam kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ya namna bora ya kutumia nyenzo hiyo.

Mhagama alisema Umoja wa Afrika (AU) umeliheshimisha taifa kwa kutoa fursa ya kuwa nchi ya kwanza Afrika kufanyiwa majaribio ya kutumia nyenzo hiyo ambayo itaziwezesha nchi wanachama kuandaa taarifa itakayokuwa ikizingatia misingi iliyoainishwa kwenye mkataba huo.

Alisema nchi wanachama wa AU zilikubaliana kutengeneza nyenzo ambayo itatumika kusaidia kupima utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Maadili na Misingi ya Utumishi wa Umma na Utawala katika nchi zote wanachama.

Aliongeza kuwa mkataba huo unahimiza uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma katika maeneo mbalimbali likiwamo eneo la mapambano dhidi ya rushwa, uzingatiaji wa sheria na utawala bora kwa ujumla.

Waziri Mhagama alisema semina hiyo ni fursa ya kipekee kwa watendaji wa pande zote mbili za Muungano kwenye ofisi zinazoshughulikia masuala ya utumishi wa umma kuangalia ni kwa namna gani wataitumia nyenzo hiyo vizuri katika kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Umoja wa Afrika.

"Jambo kubwa hapa ni nchi yetu kuwa ya kwanza kuitumia nyenzo hiyo, kupata mafunzo ya kuitumia pamoja na kuwa wa kwanza kutathminiwa kwa namna gani tumeitumia kuandaa taarifa itakayowasilishwa Umoja wa Afrika," aliongeza.

Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji Sera, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambaye idara yake ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa mkataba huo, Agnes Meena, alisema baada ya kukamilika kwa semina hiyo, wanatarajia kuandaa taarifa nzuri ya nchi itakayokuwa ya kwanza Afrika kwa kutumia nyenzo hiyo.

Naye mshiriki wa semina hiyo kutoka Tanzania Bara, Romwald Rwamarumba, alisema Tanzania imekuwa nchi ya kwanza Afrika kufanyiwa majaribio ya kutumia nyenzo hiyo, hivyo taarifa itakayoandaliwa na nchi itakuwa ya kwanza barani Afrika ilizozingatia misingi iliyowekwa kwa mujibu wa mkataba.

Alisema taarifa hiyo itatumiwa pia na nchi wanachama barani Afrika kama rejea ya uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa mkataba huo kwenye nchi zao.

Mshiriki kutoka Zanzibar, Fatma Saadalla, alisema semina hiyo itasaidia kuwajengea uelewa wa mkataba huo na namna ya kutumia nyenzo iliyopendekezwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Maadili na Misingi ya Utumishi wa Umma na Utawala.

Semina hiyo ya siku nne imeandaliwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na imewashirikisha wajumbe kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.




Ofisa Ubunifu wa Shirika lisilo la Kiserikali Tanzania Open Map Development, Digna Mushi (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi, kuhusu ndege zisizo na rubani 'dron' zinazotengenezwa na shirika hilo, wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya Wiki ya Ubunifu Tanzania inayoratibiwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wajawazito walazwa wodi moja na wagonjwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJAWAZITO katika Zahanati ya Chibe Manispaa ya Shinyanga, wamedaiwa kujifungua katika jengo moja na wagonjwa wa kawaida.

Imedaiwa kuwa wajawazito hao wanapokuwa wanajifungua na kupiga kelele, husikiwa na wagonjwa na maneno ambayo huyatoa wanapokuwa wakisukuma watoto sababu ya uchungu, wagonjwa huanza kuwajibu.

Diwani wa Chibe, John Kisandu, alibainisha hayo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani Manispaa ya Shinyanga, wakati akiwasilisha taarifa ya kata hiyo.

Alisema wajawazito katika Zahanati ya Chibe wamekuwa wakipata shida wakati wa kujifungua, sababu ya kutumia jengo moja na wagonjwa, ambao huwasikia wakati wa kujifungua na kuanza kujibizana maneno ambayo huyatoa jambo ambalo si zuri.

"Zahanati ya Chibe ina jengo moja tu hilohilo lihahudumia wagonjwa na kujifungua wajawazito. Naomba sana hili liangaliwe na kujengwa jengo lingine kwa ajili ya kujifungua kinamama tu," alisema Kisandu.

"Siku moja nilikuwa nikipata matibabu katika zahanati hiyo, nikasikia mwanamke akilia kwa uchungu wakati akijifungua huku akitamka maneno kuwa wanaume wote wauawe, lakini wanawake wenzake walianza kumjibu kuwa auawe wa kwako tu," aliongeza Kisandu.

Nao madiwani walipokuwa wakiwasilisha taarifa zao za kila kata, walilalamikia kukabiliwa na tatizo la ukamilishaji wa maboma ya afya, uchakavu miundombinu ya shule, barabara, matundu ya vyoo pamoja na uhaba wa watumishi.

Naye Meya wa Manispaa wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema kero zote ambazo zimewasilishwa na madiwani kupitia taarifa zao za kwenye kata zifanyiwe kazi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alisema tatizo ambalo linakwamisha utatuzi wa kero hizo ni upungufu wa rasilimali fedha na kubainisha kuwa watakuwa wakizitatua moja baada ya nyingine, na hadi kufikia mwaka 2025 nyingi zitakuwa zimeshatatuliwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua za kushusha bei ya mafuta zinahitaji usimamizi

**SERIKALI** jana ilitangaza hatua mbalimbali za kupunguza bei za mafuta ifikapo Juni Mosi, mwaka huu, lengo likiwa kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi.

Kupanda kwa bei za mafuta kulitangazwa wiki iliyopita hatua ambayo imesababisha bidhaa mbalimbali kupanda gharama pamoja na usafiri wa vyombo vya usafiri, sababu kubwa ya kupanda kwa bei hizo ni vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine.

Kutokana na kupanda huko kwa bei, Bunge liliingilia kati na kuitaka serikali kupitia Waziri wa Nishati, January Makamba, kupeleka majibu ya namna ilivyojipanga kupunguza ukali wa bei ya mafuta kwa wananchi na hatimaye jana aliwasilisha taarifa hiyo.

Waziri Makamba aliweka bayana kwamba serikali imesikia kilio cha wananchi na kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa ruzuku ya Sh. bilioni 100, ilifikapo tarehe iliyoahidiwa na bidhaa hiyo iwe imeshuka bei. Nafuu nyingine, kwa mujibu wa Makamba ni kupata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) utakaopatika mwaka ujao wa fedha.

Hatua nyingine iliyochukuliwa ni kuruhusu wenye uwezo wa kuagiza na kuingiza mafuta kwa bei nafuu kufanya hivyo huku serikali ikitangaza kupunguza matumizi ya serikali kwa muda uliobaki wa mwaka wa fedha 2021/22.

Kwa uamuzi huo, serikali inastahili pongezi kwa kutekeleza jambo hilo na kuonyesha kwa vitendo kuwa ni sikivu katika kutatua kero za wananchi wake. Ni imani kwamba uamuzi huo ukisimamiwa vyema, utaleta nafuu kwa wananchi ambao wameingia kwenye ugumu wa maisha kutokana na kupaa kwa bidhaa na huduma.

Hata hivyo, ni vyema serikali ikaliangalia vyema suala la kuruhusu wafanyabiashara binafsi kuagiza mafuta nje ya nchi kwamba isigeuke kuwa adhabu baadaye kwamba wanaweza kuungana na kutengeneza uhaba wa bidhaa hiyo.

Tunatambua kwa sasa tunatawaliwa na soko huria kwamba kuna ushindani unaoamua soko ya bidhaa husika, lakini lazima kuwa na mifumo ya kusimamia ili isifike wakati ukatengenezwa uhaba wa bidhaa hiyo ili kupandisha bei.

Ni muhimu kufanya utafiti wa kina na kujifunza kutoka kwa nchi zinazofanya hivyo, kujua changamoto na fursa zilizopo ili nchi isiingie kwenye matatizo makubwa yatakayoendeleza ugumu wa maisha kuliko hali ilivyo sasa.


Pia kwenye kupunguza matumizi wananchi wanapenda kuona kwa uhalisia, kwa kuwa kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na mfumuko wa shughuli zilizorejesha utengenezaji wa sare mbalimbali na vifaa ambavyo kimsingi ukifuatilia ni fedha nyingine imetumika.

Tunatambua ni muhimu kuwa na sare, kutengeneza kalenda na vitabu, lakini tujiulize kwa hali ya uchumi wa nchi yetu ni muhimu kufanya hivyo sasa? Kwanini fedha hizo zisisaidie kuweka ruzuku kukabili changamoto ilipopo.

Tunaamini mwananchi anapopitia hali ngumu ya maisha kwasababu ya kupaa kwa mafuta, anatamani kusikia lugha ya kupooza makali kutoka kwa serikali, na ndicho kilichofanyika, lakini sasa ni muhimu kudhibiti wizi wa fedha za umma, ili zielekezwe kwenye utekelezaji wa majukumu muhimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uvumilivu kisiasa Kenya tiba kuelekea uchaguzi mkuu

Na Mwandishi Wetu

**AFRIKA** Mashariki inaitazama Kenya mmoja wa wanachama wake ikielekea kwenye uchaguzi mkuu Agosti mwaka huu na kuitakia kila la heri.

Wanapokwenda kuwachagua viongozi wao Raila Odinga au Naibu Rais William Rutto, ambao ni watiania ya urais, wana Afrika Mashariki, wanawakumbusha kuwa ni vyema kufanya juu chini ili hali ya kiuhusiano wa kidiplomasia iendelee kuwa bora.

Hata katika uongozi mpya utakaoingia madarakani miezi mitatu kuanzia sasa, ili Afrika Mashariki ibaki salama kidiplomasia, izidi upendo kati ya Rwanda, Tanzania, Burundi, Congo DRC, Sudan Kusini na Kenya.

Hivyo licha ya kuwa na mabadiliko ya uongozi siku za usoni, ni vyema kuendelea kuazimia kuwa na kufikia uhusiano mwema katika nyanja zote kuanzia biashara, uwekezaji na ujirani mwema.

Wakati huu uchaguzi unapokaribia Kenya au Rais Uhuru Kenyatta, ndiye Mwenyekiti wa EAC, hivyo jukumu ni lake kuendelea kuhakikisha Afrika Mashariki na uongozi mpya wa Kenya vinaendelea kudumishwa mshikamano.

Mwaka jana Tanzania na Kenya, zilimaliza sintofahamu za kidiplomasia na kibiashara zilizokuwa zinawazonga majirani hao, jambo ambalo linategemewa litaendelea hata katika awamu mpya ya Ruto au Odinga itakayoingia madarakani karibuni.

Uganda na Rwanda zilishawahi kushutumiana na kuzuia malori ya shehena kutoka na hata kuingia kwenye mipaka yao na hata kuufunga mpaka wa Gatuna, lakini yote hayo yalimalizika.

Pia Uganda ilijibu ikizuia raia wa Kigali kuingia nchini humo kwa sababu ya usalama wao, yote hayo sasa ni historia kwani kikubwa ni kupendana na kumaliza sintofahamu zinazokwamisha ujirani mwema.

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ya wote, ndiyo maana EAC inawatakia Wakenya uchaguzi ulio huru na haki na unaitazama kama 'kaka mkubwa' kwenye demokrasia ikiwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, iliyo huru na ya kisasa.

Aidha, Kenya ndiyo yenye mahakama au mhimili wa sheria na bunge ilio huru kuliko baadhi ya mataifa mengi ya EAC, hivyo ni rahisi wengine kujifunza kutoka kwao.

Kenya imekuwa kinara wa usuluhishi wa migogoro Afrika Mashariki na itakumbukwa kuna kipindi Uganda na Rwanda zilizozana na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, akateuliwa kuwa msuluhishi wa uhasama uliokuwa unaendelea na kupatikana suluhu.

Mafanikio yalipatikana kwa kuwa Wakenya wamekuwa na historia ya mizozo na migogoro ikiwahusisha viongozi wakuu wa kisiasa Rais na Makamu wake ambao ilifikia hatua ya kushtakiwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya ICC, lakini waliimaliza na kulileta pamoja taifa lao.

Si hivyo tu ushiriki wake wa masuala ya siasa na uchumi ndani ya EAC umekuwa wa matumaini kwa kuwa ni nchi yenye uchumi mkubwa zaidi ndani ya jumuiya.

Kenya au kaka mkubwa imekuwa mstari wa mbele kupunguza uhasama wa kisiasa kati ya Rais Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, ambaye ni mgombea urais, hivyo kwa Afrika Mashariki Kenya inaweza kuwa nyenzo ya kusaidia kusuluhisha migogoro ya ndani na ya majirani au wana jumuiya wengine.

Kenya inabaki kuwa kiongozi kiusuluhishi kwa kuzingatia namna ilivyofanikiwa kuwaunganisha Wakenya hasa baada ya Mahakama ya Juu kutengua ushindi wa Rais Kenyatta na kutaka urudiwe tena, kabla ya kushinda tena katika uchaguzi wa marudio.

Yote hayo yanaleta matumaini ya kupata mafanikio katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na kujifunza kutoka Kenya.

Afrika Mashariki inaendelea kuamini kuwa wagombea urais wa Kenya ni viongozi waandamizi katika utawala wa nchi hiyo.

Wamewahi kuwa marafiki, wakakwaruzana pia kwa nyakati tofauti wameendelea kukutana kwenye majukwaa ya kijamii na bado kazi inaendelea.

Cha kuzingatia ni kwamba kuna maisha baada ya siasa na pia jukumu la kila mmoja awe mgombea au mgombea mwenza kwenye uchaguzi mkuu ni kulinda maslahi makubwa ya taifa au Kenya na wala si haja wala maslahi ya mgombea au mtu mmoja na chama chake.

HABARI KITAIFA

## Mwinyi apongeza ushirikiano madhehebu ya dini

**Na Mwnadishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza ushirikiano baina ya madhehebu ya dini ambao umewawezesha wananchi kuishi kwa amani na upendo bila kujali imani zao.

Sambamba na pongezi hizo amesisitiza kuwa ili taifa liwe na amani, ni lazima wananchi wake wapate haki za msingi.

Dk. Mwinyi alisema hayo katika sherehe za Jubilee ya Miaka 25 ya Askofu wa kanisa Katiliki Jimbo la Zanzibar, Mhashamu Augustine Shao, iliofanyika katika Uwanja wa Amani, Zanzibar.

Alitumia fursa hiyo kuwahimiza wananchi kuendelea kudumisha amani iliyoko nchini, ikiwa ni utamaduni uliozoeleka wa kuishi kwa amani na kuvumiliana miongoni mwa watu wenye imani tofauti za kidini.

Alisema Zanzibar ina historia ya muda mrefu ya wananchi wake kuishi kwa kuvumiliana kidini, jambo linaloiletea sifa kubwa nchi, sambamba na kuliwekea taifa msingi muhimu wa umoja.

Dk. Mwinyi alipongeza uamuzi wa Kanisa Katoliki Zanzibar kwa ushirikiano na viongozi wengine wa dini katika Kamati ya Kitaifa ya Amani inayojumuisha madhehebu tofauti ya dini na kusema ushirikiano huo unatoa nafasi kubwa ya kuimarisha umoja wa taifa katika kushajiisha maendeleo na ustawi wa jamii.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inathamini mchangao wa viongozi wa dini katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo na kubainisha azma ya kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote zinazohusu masuala ya ajira, usafirishaji wa binadamu, ukwepaji kodi pamoja na uimarishaji wa huduma za wagonjwa wanaoishi Kituo cha Wazee Welezo.

Rais Mwinyi alisema anatambua mchango mkubwa wa taasisi za dini katika kuwahimiza waumini juu ya utii wa sheria na kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani, ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya, vitendo vya udhalilishaji, huku akipongeza taasisi za kidini kwa kuwa mstari wa mbele katika kusimamia maadili na ustawi wa jamii.

"Tunathamini na kutambua mchango wa taasisi za kidini katika uimarishaji wa huduma za kijamii. Napenda niwaahidi serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi za dini ili kutoa huduma mbalimbali kwa ufanisi zaidi", alisema.

Alisema ili taifa liwe na amani, ni vyema likahakikisha kila mwananchi anapata haki zake za msingi, hivyo akaahidi kuzipatia ufumbuzi wa haraka changamoto mbalimbali zinazolikabili kanisa.

Dk. Mwinyi aliwataka viongozi wote wa dini katika madhehebu tofauti kuwa waadilifu kwa kigezo kuwa hatua hiyo itawaletea sifa, sambamba na kuwajengea imani waumini wao.

Kuhusu sera ya uchumi wa bluu na utekelezaji wake, Dk. Mwinyi alisema serikali imegawa dhana hiyo katika sekta kuu tano ambazo ni utalii, bandari, biashara na usafirishaji, uvuvi, mwani pamoja na mafuta na gesi.

Alisema utalii ni mhimili wa uchumi wa taifa na kwamba asilimia 30 ya pato la taifa inategmea utalii, hivyo akabainisha malengo ya serikali kuwa ni kutumia vyema rasilimali za bahari katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema kilimo cha mwani na uvuvi ni eneo linalochukua theluthi mbili ya watu, hivyo serikali imeweka mkazo katika uimarishaji wa zana za uvuvi, ili kuimarisha uzalishaji na kuwaondolea wananchi umasikini.

Pia alisema serikali ya awamu ya nane imeanzisha ujenzi wa bandari kubwa ya kisasa katika eneo la Mangapwani, itakayohusisha bandari tofauti, kwa lengo la kuongeza pato la taifa.

Dk. Mwinyi alisema eneo lingine lililoko katika sekta hiyo ni mafuta na gesi na kubainsiha kiwango kikubwa cha gesi kilichokwisha kugunduliwa na wataalamu hadi sasa.

Alisema biashara na usafirishaji baharini ni eneo ambalo bado halijafanyiwa biashara ya kutosha na kusema serikali ina azma ya kuimarisha biashara baharini ili kuchochea uchumi wake.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan, aliahidi kuzifanyia kazi changamoto zote zilizowasilishwa na viongozi mbalimbali sambamba na kuahidi kuendeleza ushirikiano na viongozi na waumini wa dini hiyo bila ubaguzi.

Askofu Shao pamoja na mambo mengine, aligusia uwepo wa changmoto mbalimbali zinazolikabili kanisa na waumini wake.

Alisema Katiba ya Zanzibar inawapa haki ya kumiliki ardhi wananchi wote bila ubaguzi wa kidini au eneo mtu anakotoka, jambo ambalo limekuwa kinyume kwa waumini wa dini hiyo.

Askofu Shao alisema kanisa linakabiliwa na changamoto katika suala la upatikanaji wa vibali vya utoaji huduma na kusema wamisionari hawawezi kutekeleza kazi za maendeleo ya jamii bila ushirikiano na kubainisha kuwa jamii ya Wanzibari ni watu wapole, hivyo akaomba hali hiyo iende sambamba na upatikanaji wa fursa ili watu wengi wafanye kazi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (kulia), akizungumza baada ya kutembelea kiwanda cha ngozi cha Sintakwame Investment, Kurasini mkoani Dar es Salaam jana, kinacholalamikiwa na wakazi wa eneo hilo kutoa harufu kali na kuwasababishia usumbufu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shahidi aeleza jinsi walivyoshambuliwa mateke na wafuasi wa Zumaridi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHAHIDI wa kwanza kati ya 20 wanaotarajiwa kutoa ushahidi katika kesi inayomkabili Mchungaji Diana Bundala, maarufu kama Zumaridi, ameanza kutoa ushahidi wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza.

Kesi hiyo namba 10 ya mwaka 2022 ya kufanya shambulio la kudhuru mwili kwa lengo la kuzuia maofisa wa serikali kutimiza wajibu wao linalomkabili Zumaridi na wenzake wanane, ilianza kutolewa ushahidi jana.

Shahidi huyo ambaye ni Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Christina Mwisongo (46), alitoa ushahidi huo akiongozwa na Wakili wa Serikali, Emmanuel Luvinga.

Katika ushahidi wake, Mwisongo alidai kuwa Februari 22, mwaka huu, alipokea amri ya Mahakama ya Mwanzo Mkuyuni ya kumtaka aende nyumbani kwa Zumaridi kuchukua mtoto (jina limehifadhiwa).

Alidai kuwa mtoto huyo alikuwa akiishi na mama yake mzazi nyumbani kwa Zumaridi.

Kabla ya hapo aliambia mahakama kwamba nakala ya hukumu hiyo ya mahakama alipewa na Wakili Linus Munishi pamoja na Ally Abbas ambaye ni baba wa mtoto huyo.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya kufika nyumbani kwa mchungaji huyo akiwa ameongoza na askari polisi, hawakufunguliwa geti la nyumba hatua iliyowafanya kupitia mlango wa nyuma na kuingia ndani.

Alidai kuwa baada ya kufika hawakupewa ushirikiano wa kutosha na wakaamua kuingia ndani na kuwakuta watu sebuleni wakiwa wanasali na ikawabidi wasimame na kusubiri wamalize kusali.

Mwisongo alidai kuwa baada ya mchungaji huyo na waumini wake kumaliza kusali, walianza kuunguruma kama simba na kunyanyuka huku wakitembea mwendo wa ajabu hali iliyowafanya waogope na kutoka nje.

Shahidi huyo alidai kuwa watu hao wakiwa na Zumaridi, walimkamata askari mmoja aliyetajwa kwa jina la James na kuanza kumvuta, kumkanyaga na kumpiga mateke huku wakiendelea kunguruma.

Shahidi aliendelea kudai kwamba baada ya hapo walishikwa na taharuki wakamwacha James ambaye aliendelea kujiokoa na kufanikiwa kutoka na wote wakatoka katika lango hilo na kushindwa kutekeleza amri ya mahakama.

Licha ya kutoka nje, shahidi huyo alidai kuwa washtakiwa hao waliendelea kuwashambulia kwa kuwarushia vitu mbalimbali vikiwamo viti.

Kutokana na hali hiyo, alidai kuwa waliamua kutoka nje ya geti na kuingia katika gari.

Wakili wa utetezi, Erick Mutta, akimhoji shahidi huyo, alimuuliza kama kabla ya kuingia katika nyumba hiyo alionana na uongozi wa mtaa huo.

Akijibu swali hilo, shahidi huyo alikiri kufika nyumbani kwa mchungaji huyo bila kupitia serikali ya mtaa na kwamba yeye alikuwa anaongozwa na askari James.

Aidha, wakili huyo alimuuliza shahidi ni kwa nini alikwenda kanisani kwa Mchungaji Diana, badala ya nyumbani kwa mama wa mtoto huyo kama amri ya mahakama ilivyoelekeza.

Shahidi huyo alijibu kwamba walimuuliza baba wa mtoto huyo na kuambiwa kwamba mwanawe kwa wakati huo alikuwa kwa Mchungaji Diana.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Monica Ndiyokobora.

Inadaiwa kuwa Februari 23, mwaka huu, katika eneo la Buhongwa wilayani Nyamagana mkoani Mwanza, washtakiwa hao kwa pamoja walimshambulia askari James Mgaya katika sehemu mbalimbali za mwili na kumzuia ofisa wa umma kutekeleza majukumu yake.

Awali, mahakama hiyo ilielezwa kuwa siku ya tukio, askari huyo pamoja na Ofisa Ustawi wa Jamii, Mwisongo, walifika nyumbani kwa mshtakiwa namba moja, Zumaridi, kwa ajili ya kuchukua mtoto wa Ali Abbas Shabani ambaye ni mzazi mwenzake na mshtakiwa namba sita katika kesi hiyo.

Wakili wa Serikali, Emmanuel Luvinga, alidai kuwa washtakiwa hao walianza kuwashambulia akiwamo askari Mgaya na kumzuia kutimiza majukumu yake kama alivyoagizwa na Mahakama ya Mwanzo ya Mkuyuni.

# Kampuni 100 za EU zawekeza Tanzania

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema inajivunia uhusiano na ushirikiano imara kati yake na Umoja wa Ulaya (EU), ikibainisha kuwa mpaka sasa zaidi ya kampuni 100 kutoka nchi wanachama wa umoja huo zimewekeza Tanzania.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alitoa kauli hiyo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Ulaya.

Balozi Mulamula alisema EU imesimama na Tanzania wakati wote na imeendelea kuunga mkono ajenda ya maendeleo.

"Serikali ya Tanzania inaushukuru Umoja wa Ulaya kwa uhusiano huu imara ambao umedumu kwa muda mrefu pamoja na msaada ambao umekuwa ukitolewa kwa miaka mingi.

"Umoja wa Ulaya ni wadau wetu wakubwa wa maendeleo, wanagusa kila sekta, mwezi Februari mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alitembelea makao makuu ya Umoja wa Ulaya, Brussels na alikutana na wafanyabiashara, tulipata ahadi ya kampuni nyingi zilionyesha nia ya kuja kuwekeza Tanzania," alisema.

Waziri huyo alisema hadi sasa wana kampuni zaidi ya 100 kutoka nchi za EU ambazo zimewekeza Tanzania na wawekezaji wengi kutoka nchi za Jumuiya ya Umoja wa Ulaya zimeonyesha nia ya kuwekeza nchini na wameridhishwa na mazingira ya biashara yaliyopo.

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti, alisema wataendelea kushirikiana na Tanzania kuimarisha maendeleo katika sekta ya biashara na uwekezaji, utamaduni, uongozi kwa wanawake katika masuala ya siasa, elimu na afya kwa maslahi ya mataifa yote mawili.

"Tunaiona Tanzania ikiendelea kubadilika mara kwa mara tunakutana na vijana na watu wenye vipaji wakitekeleza malengo na miradi yao, hivyo muundo wa kijamii unabadilika.

"Hii ni dhahiri kabisa kuwa Watanzania ndiyo waamuzi wa mustakabali wa jamii yao, Umoja wa Ulaya utaendelea kuunga mkono jitihada za mabadiliko katika jamii ya Watanzania kwa kuwa huo ndiyo ushirikiano na urafiki,"Balozi Fanti alisema.

Balozi Fanti pia aliipongeza Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuongeza mwanachama mpya ambaye ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kwa kuwa jambo hilo ni jema na linaongeza nguvu ya ushirikiano katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema Umoja wa Ulaya utaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika kukuza na kuendeleza uchumi wa mataifa hayo kwa maslahi ya pande zote mbili.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui aliyemwakilisha Rais wa Umoja wa Ulaya katika maadhimisho hayo, alisema Jumuiya ya Ulaya imelenga pamoja na mambo mengine, kuendelea kuimarisha ushirikiano na Tanzania, kuongeza mshikamano, amani na uhuru pamoja kukuza demokrasia.

Katibu Mkuu Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Dk. Peter Mathuki, alisema Umoja wa Ulaya umekuwa mshirika mkuu wa nchi wanachama wa EAC kutokana na uhusiano mzuri na wa kihistoria uliojengewa misingi imara tangu 1975.

"EAC tunaishukuru Jumuiya ya Umoja wa Ulaya kwa misaada endelevu kwa miradi na programu za Jumuiya yetu ambazo zimekuwa zikiwanufaisha wananchi kwa miaka mingi," Dk. Mathuki alisema.

Pia alizipongeza nchi wanachama wa Jumuiya Umoja wa Ulaya kwa umoja ambao umekuwa mfano wa kuigwa wa kiuchumi duniani kote.




Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Kaanaeli Nnko (kulia), alipotembelea banda la TADB, wakati wa Maonyesho ya tano ya mifuko na programu za uwezeshaji Kitaifa, katika uwanja wa Jamhuri, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika aonya wabunge kuhusu kudhalilishana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka wabunge kuheshimiana baada ya Mbunge wa Sengerema (CCM), Hamisi Tabasamu, kutoa maneno ya kumdhalilisha mbunge aliyezungumzia kurasimisha na kuzipima pombe za kienyeji, ikiwamo gongo.

Dk. Tulia alitoa onyo hilo jana bungeni jijini hapo kufuatia mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara, ambapo alidai kuwa Mbunge Tabasamu alimdhalilisha nje ya Bunge juzi Mbunge wa Momba (CCM), Condester Sichalwe, kwa kumwita 'mbunge wa ajabu' kutokana na mchango alioutoa wakati akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/23 juzi.

Katika mwongozo wake, Dk. Ntara alisema Sichalwe alitoa taarifa kwa Katibu wa Bunge kuwa atachangia na atafanya ulinganifu wa pombe za kisasa na pombe zinazozalishwa nje ya nchi wakati wa kuingiza vifaa hivyo bungeni, taratibu zote za usalama zilizingatiwa.

"Pombe zilikabidhiwa kwa wasaidizi wa makatibu wa Bunge ambao walihifadhi na jana (juzi) chupa za pombe husika zililetwa wakati wa mchango wa Condester, alikabidhiwa na baada ya mchango zilirejeshwa kwa Katibu wa Bunge na kuhifadhiwa, hakutukana, hakuvunja sheria, hakudhalilisha mtu.

"Hakukuwa na uhalali Tabasamu kumdhihaki na kumshambulia, kauli yake ingilia uhuru wa majadiliano ya Bunge na kudhalilisha mamlaka ya kiti husuan kiongozi aliyekuwa akiongoza kikao husika kwamba aliruhusu mambo yasiyo ya maana kujadiliwa bungeni, amekiuka kanuni za Bunge kwa kuwa kanuni inasema kama mbunge hajaridhika na jambo, anasimama mahala pake na kuomba kuhusu utaratibu au mwongozo wa spika," alisema.

Spika alisema Mbunge Tabasamu hakufuata utaratibu wa kibunge na kuzungumza maneno 'mbunge wa ajabu', jambo ambalo limemwathiri kisaikolojia mbunge mwenzake na kuomba spika kutoa mwongozo wake.

Kuhusu mwongozo huo, Spika Tulia alisema asitokee mbunge wa kumdhalilisha mwenzake ndani wala nje ya Bunge na hakuna mbunge wa ajabu, wote wana heshima sawa.

"Katiba inalinda uhuru wa mawazo humu ndani inaangalia ukubwa wa nchi yetu tofauti za jimbo moja na lingine na shughuli za wananchi wanazozifanya kwenye maeneo husika.

"Ni kazi yangu kuwalinda wabunge ndani na nje pia, asitokee mbunge wa kumdhalilisha humu ndani wala nje, humu ndani hakuna mbunge wa ajabu, wote wana kiapo kimoja na heshima sawa sawa," alionya.

Alisema wabunge wanalipwa mishahara ambayo baadhi ya kodi zake zinatokana na mauzo ya pombe na kwamba Bunge limekuwa likikagua viwanda vya pombe na hakuna biashara itakayosemwa na kuonekana mbunge wa ajabu.

Alisema biashara hiyo inafanywa na wanawake wa jimbo hilo, hivyo ni wajibu wa mbunge kuwatetea bungeni na kumtaka mbunge kuwa na amani.

## Nape awapa jukumu nyeti maofisa habari

**Na Christina Haule,** TANGA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amewataka maofisa habari na mawasiliano kuhakikisha tovuti na mitandao ya kijamii za taasisi zao zinatangaza vivutio vya utalii ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan.

Aprili 28, mwaka huu, Rais Samia alizindua filamu ya The Royal Tour yenye lengo la kutangaza utalii uliopo Tanzania kimataifa na kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza maeneo tofauti na kukuza uchumi.

Akizungumza juzi katika uzinduzi wa mkutano wa 17 wa maofisa habari, mawasiliano na uhusiano wa serikali uliofanyika mkoani Tanga, Waziri Nape alimpongeza Rais Samia kwa jitihada zake za dhati za kufungua sekta ya utalii na kuwataka maofisa hao kuwa sehemu ya mkakati wa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Kaimu Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Twaha Twaibu, alisema wameshiriki mkutano huo kwa lengo la kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana kwenye mapori ya Akiba na mapori Tengefu.

Akizungumzia kauli ya Waziri Nape ya kutoa siku 14 kwa maofisa habari kutumia tovuti na mitandao ya kijamii, Twaibu alisema wameipokea na wataifanyia kazi ili kutangaza zaidi vivutio vya utalii vilivyopo.

Mkutano huo umeshirikisha wadau wa habari, mawasiliano na teknolojia ya habari kutoka taasisi mbalimbali za serikali Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.





# Ajira za makarani wa sensa zavutia wengi

Na Paul Mabeja, DODOMA

SERIKALI imesema mwenendo wa uombaji wa ajira za muda za makarani na wasimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi unaendelea vizuri ambapo hadi juzi, jumla ya watu 119,468 walikuwa wameshatuma maombi.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapo, alisema kati ya waombaji hao, 46,159 ni waajiriwa kutoka sekta ya umma na binafsi.

Alisema waombaji wengine 14,393 ni wale ambao wameajiri katika sekta mbalimbali na waombaji 58,916 ni wale ambao hawana ajira yoyote.

"Mei 5, mwaka huu, serikali ilitangaza rasmi kuanza kupokea maombi ya kazi za muda za makarani na wasimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, kupitia mfumo wa kielektroniki, mwenendo wa uombaji unaendelea vizuri nchi nzima," alisema Dk. Chuwa.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya dosari ambazo waombaji wamekuwa wakikumbana nazo ikiwamo kutokujaza taarifa sahihi kama barua pepe na namba za simu na hivyo kushindwa kupokea neno la siri na taarifa nyingine muhimu.

Alitaja shida nyingine ni waombaji kusahau jina la mtumiaji na neno la siri, hivyo kushindwa kuhuisha fomu namba moja iliyoidhinishwa na mwajiri kwa waajiriwa na viongozi wa serikali za mitaa.


Dosari nyingine ni baadhi ya waombaji kukosa baadhi ya taarifa kama vile namba ya Kitambulisho cha Taifa na cheti cha kuzaliwa.

"Waombaji wote wanatakiwa kuwa makini wakati wa kuingia katika mfumo na kusoma maelekezo kabla ya kuanza kujaza fomu na kuhakikisha taarifa zinajazwa kwa usahihi kuondoa usumbufu wa kuhuisha taarifa mara kwa mara.

"Waombaji wanatakiwa kujaza namba ya simu na barua pepe ambayo inatumika wakati wote ili aweze kupokea taarifa za akaunti yake ya kuingia katika mfumo mapema iwezekanavyo," alisema.

Vilevile, aliwataka waombaji kuandaa viambatanisho muhimu kama cheti cha kuzaliwa, cheti cha kidato cha nne na namba ya NIDA ili wakati wa kujaza fomu wasikwame.

Alisema fomu ya maombi ya kazi ya sensa inapatikana bila malipo na waombaji wote watatakiwa kutuma maombi kabla ya Mei 19, mwaka huu saa sita usiku.



Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonaz (wapili kulia), akishuhudia Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Sitholizwe Mdlalose (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Mhandisi Peter Ulanga, wakibadilishana mikataba ya kununua huduma za mkongo wa Taifa kati ya Vodacom na Mkongo wa Taifa (NICTBB) wenye uwezo wa 10Gps kwa thamani ya Sh. bilioni 23.2, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi wa Sheria wa TTCL, Anita Moshi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Viongozi wa dini wajiendeleze kielimu'

Na Peter Mkwavila, DODOMA

KATIBU Mkuu wa Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekosti Tanzania, Askofu Baraka Kihonza, amewataka viongozi wa dini kuwa na tabia ya kujiendeleza kitaaluma kwa kusoma sheria ili kuepukana kutoa mafundisho ya upotoshwaji kwa jamii.

Askofu huyo alisema hayo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya sheria na utawala, katiba na kuandaa mchanganuo wa miradi na mikakati kwa viongozi wa dini ngazi ya maaskofu na wachungaji jijini Dodoma.

Alisema wakisoma sheria na katiba itawawezesha kuepukana na mafundisho yanayopotosha jamii na kusababisha kuwapo kwa Watanzania wasiokuwa na uelewa.

Alisema kuwa elimu hiyo ni muhimu kuijua kwa viongozi wa dini, kwa kuwa itasaidia hata kwa serikali katika kutatua baadhi ya migogoro inayojitokeza ikiwamo suala zima la mirathi.

Katibu huyo alisema kuwa pamoja na kusoma vitabu vitakatifu ambavyo pia ni sehemu ya katiba, itawawezesha kuwaandaa Watanzania ambao watazijua sheria za nchi na kuzilinda.

Mratibu mkuu wa mafunzo hayo yaliyokuwa yameandaliwa na Chuo cha Paradise Christian University chenye makao yake mkoani Mwanza, Askofu Prof. Peter Watae, alisema viongozi hao wa dini watasaidiwa kutambua sheria za msingi kwa ajili ya kuwasaidia waumini wao kupitia mafunzo hayo.

Prof. Watae alisema viongozi hao watapata elimu ya viwango vya juu itakayowasaidia kupata elimu ya ujasiri na kukemea maovu na kuibadilisha Tanzania kuwa ya misingi ya madili.

Aliwataka viongozi hao wa dini kujiendeleza kitaaluma zaidi kwenye vyuo ambavyo vinatambuliwa na serikali kisheria pamoja na kanisa.

# Mchango wa makandarasi kiuchumi kujadiliwa siku 2

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB) inatarajia kukutanisha makandarasi na wadau mbalimbali wa sekta ya ujenzi mkoani Dodoma kwa ajili ya kujadili mchango wa makandarasi katika uchumi wa Tanzania.

Mkutano huo wa siku mbili utafanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Center mkoani Dodoma tarehe 12 na 13 mwezi huu.

Kwa mujibu wa Msajili wa Bodi hiyo, Rhoben Nkori, mkutano huo utawashirikisha wadau wote wakiwamo waajiri, wataalamu washauri, wahandisi na wabunifu majengo.

Aliwataja wengine kuwa ni wakadiriaji majenzi, watunga sera za uwezeshaji wananchi kiuchumi na wataalamu mbalimbali katika sekta ya ujenzi.

"Mkutano huu wa kushauriana ambao unafanyika kila mwaka ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta ya ujenzi kwa ujumla wake. Wataalamu wa sekta mbalimbali wanakaribishwa kujisajili mapema ili washiriki katika mkutano," alisema Nkori.

Alizitaja mada zitakazotolewa kwenye mkutano huo kuwa ni mchango wa makandarasi katika uchumi wa Tanzania na vikwazo vinavyoathiri mchango wa makandarasi katika uchumi wa nchi.

Alitaja mada zingine kuwa ni masuala ya kodi na kuzingatiwa kwa makandarasi ili kuboresha mchango wao katika uchumi wa taifa na fursa katika sheria na kanuni za ununuzi wa umma kuwezesha mchango wa makandarasi wa ndani.

Alitaja mada zingine zitakazotolewa kuwa ni utatuzi wa migogoro katika ununuzi wa umma na kwamba kwenye mkutano huo pia kutakuwa na maonyesho ya teknolojia, huduma na vifaa vya ujenzi.

Akizungumza kuhusu maonyesho, Nkori alisema CRB inayakaribisha mashirika na kampuni mbalimbali binafsi na ya umma kwenda kuonyesha teknolojia, bidhaa, vifaa na zana za ujenzi.

"Mkutano utakuwa na wadau wengi wa sekta ya ujenzi, hivyo tunawakaribisha watu binafsi na mashirika kuja kuonyesha bidhaa walizonazo kwa washiriki wa mkutano huu wa mwaka," alisema Nkori.

Kaulimbiu ya mwaka huu ya mkutano huo ni 'umuhimu na mchango wa makandarasi katika uchumi wa Tanzania'.

# Serikali yaanika kiini matukio moto sokoni

SERIKALI imetaja sababu tatu za wimbi la matukio ya moto kwenye masoko katika maeneo mbalimbali nchini.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alianika kiini cha matukio hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Paresso.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kauli ya serikali juu ya matukio hayo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sagini alisema hivi karibuni kumekuwa na matukio ya moto katika baadhi ya masoko nchini na uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na vyombo vingine umebaini sababu mbalimbali za matukio hayo.

Alitaja sababu hizo ni pamoja na uunganishwaji holela wa mifumo ya umeme, kutokuzingatia tahadhari za moto kwa mama lishe na baba lishe na shughuli za uchomeleaji holela wa vyuma katika masoko.

Sagini alisema katika kukabiliana na vyanzo vya matukio hayo, umefanyika ukaguzi wa kinga na tahadhari ya majanga ya moto sambamba na utoaji wa elimu na mafunzo ya matumizi ya vifaa vya awali vya kuzima moto katika masoko nchini. Alisema serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inashirikiana na halmashauri zote kuboresha miundombinu ya kuzima moto katika masoko.

Pia alisema kuhakikisha ramani za masoko mapya zinakaguliwa na zinakidhi vigezo vya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto.

"Serikali inaendelea kusisitiza uwapo wa vifaa vya awali vya uzimaji moto, uwapo wa ulinzi wa masoko kwa saa 24 na kuzingatia utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa maalum za ukaguzi zinazotolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,"alisema.

Akiuliza swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema matukio ya kuungua masoko yamekuwa yakitokea kwa masoko ambayo hayajajengwa kisasa kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu ya kuzima moto.

"Kwa kuwa serikali imekuwa ikikusanya kodi kwenye masoko, je, haioni umuhimu wa kuwalipa fidia wafanyabiashara ambao vitu vyao vimeungua kwenye masoko hayo?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema suala la fidia ni la kisheria na Bunge halijapitisha utaratibu wa aina hiyo.

"Hata hivyo, lililo la muhimu ni elimu ya kinga dhidi ya majanga haya ili yasitokee kwenye maeneo yetu, na tumeanza kutoa mafunzo ili kuwezesha kujikinga na majanga ya moto," alisema.



Waziri wa Nishati, January Makamba, akiwasilisha taarifa kuhusu kupanda kwa gharama za mafuta nchini, Bungeni jijini Dodoma jana, alisema serikali itaweka ruzuku ya Sh. bilioni 100 ili kukabiliana na ongezeko la bei za mafuta duniani.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bilioni 80/- kujenga nyumba za walimu

SERIKALI imesema kwa mwaka wa fedha 2022/23, imetenga Sh. bilioni 81.48 kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Segerea (CCM), Bonnah Kamoli.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa vitendo kwa kuhakikisha inajenga nyumba za walimu kama inavyofanya kwa majeshi ya ulinzi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alifafanua kuwa kati ya fedha hizo Sh. bilioni 37.85 ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za sekondari na Sh. bilioni 43.63 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za msingi.

Alisema serikali inatambua tatizo la mahitaji ya nyumba za walimu nchini na ili kutekeleza Ilani ya CCM kwa vitendo, serikali itaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ikiwamo ujenzi wa nyumba za walimu kulingana na upatikanaji wa fedha kupitia vyanzo mbalimbali.

Naibu Waziri huyo alisema serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya nyumba za walimu katika maeneo ambayo kuna uhitaji mkubwa likiwamo na Jimbo la Segerea kadri fedha zitakavyopatikana.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alihoji kwanini serikali isibadili utaratibu wake na kupeleka nyumba hizo kwa majimbo badala ya kutumia mfumo.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema serikali imejizatiti kutatua tatizo hilo kwa kutenga fedha na itazingatia maeneo yote yenye uhaba ikiwamo jimboni kwake.

Katika swali lake, Mbunge wa Chemba (CCM), Mohamed Moni, alisema Wilaya ya Chemba ina shule za msingi 103 na asilimia 70 ya shule hizo zipo vijijini na ni vigumu kupata nyumba za kupanga.

"Mna mkakati gani wa makusudi wa kujenga nyumba kwenye shule hizo?" Alihoji.

Silinde, akijibu swali hilo, alisema mkakati wa serikali ni kujenga nyumba maeneo ya pembezoni na kwamba pamoja na kutenga fedha, kuna miradi mbalimbali inatekelezwa na itazingatia mahitaji ya wilaya hiyo.

## Mbunge aona shida soko la maziwa nchini

MBUNGE wa Busanda (CCM), Bryceson Tumaini, amehoji mkakati wa serikali kushughulikia soko la ndani la maziwa.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mkakati gani wa kuhimiza na kuhamasisha unywaji wa maziwa shuleni kabla ya kutafuta masoko ya nje.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema serikali imeendelea na mkakati wa kukuza soko la maziwa nchini kwa kuimarisha na kuendeleza programu mbalimbali zinazochochea unywaji wa maziwa nchini ikiwamo programu ya unywaji wa maziwa shuleni.

Alisema mpango wa unywaji maziwa shuleni umewafikia watoto 90,000 wa shule za msingi 39 katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mbeya, na Tanga.

Vilevile, alisema serikali inaendelea kuhamasisha unywaji maziwa nchini kwa kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, maonyesho mbalimbali na Wiki ya Maziwa Kitaifa inayoadhimishwa mwezi Mei kila mwaka.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali itakutana na wadau mbalimbali, wakiwamo wa maziwa, ili kuandaa mikakati thabiti kwa lengo la kuongeza idadi ya shule zinazotoa huduma ya unywaji maziwa.




**Habari zote na Augusta Njoji**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF FAUSTINE MKENDA (MB) ILIYOWASILISHWA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23



**Mhe. Prof. Adolf F. Mkenda (Mb)**
WAZIRI



**Mhe. Omary J. Kipanga (Mb)**
NAIBU WAZIRI



**Prof. Carolyne I. Nombo**
NAIBU KATIBU MKUU



**Prof. Eliamani M. Sedoyeka**
KATIBU MKUU



**Prof. James E. Mdoe**
NAIBU KATIBU MKUU





# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF FAUSTINE MKENDA (MB) ILIYOWASILISHWA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23

**A. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na muda naomba hotuba yangu iingie kwenye taarifa rasmi za bunge (hansard) kama ilivyowasilishwa.

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 la Tume ya Taifa ya UNESCO, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, kuniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila kitu, hasa kwa amani na mshikamano wa Taifa letu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumshukuru sana **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwa kuendelea kumuamini Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) kuwa Naibu Waziri. Napenda pia kumshukuru Rais kwa uongozi na miongozo anayotupatia ambayo imetusaidia sana katika kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nawashukuru pia **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais,** na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Rais katika kutusimamia na kutuongoza.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe, **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb)** kwa uongozi wako mahiri wa Bunge letu tukufu. Nawashukuru pia **Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)** na wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao. Nakupongeza pia Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Nampongeza pia **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika na kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza waheshimiwa wabunge wafuatao; Hayati Elias John Kwandikwa aliyekuwa Mbunge wa Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliyefariki tarehe 2 Agosti, 2021, Hayati William Tate Ole Nasha aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji, aliyefariki tarehe 27 Septemba, 2021, na Hayati Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Rukwa aliyefariki tarehe 24 Aprili, 2022. Natoa pole kwa ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu, na kwa namna ya pekee natoa pole kwa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe (Mb) kwa kufiwa na mtoto wake; naungana na familia, ndugu, jamaa na marafiki kumuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimshukuru kwa namna ya pekee Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb),** Makamu Mwenyekiti, **Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mb),** na wajumbe wote wa Kamati kwa kuchambua na kuishauri Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/23. Kamati hii ni makini sana, na imekuwa ikitoa maoni na ushauri wenye lengo la kuhakikisha tunaendelea kuboresha elimu na kuendeleza sayansi na teknolojia kwa manufaa ya Taifa letu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda pia kuwapongeza wabunge waliochaguliwa hivi karibuni kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni **Mheshimiwa Emmanuel Leklshon Shangai (Mb)** wa Jimbo la Ngorongoro na **Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani (Mb)** wa Jimbo la Ushetu. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha** kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kumshukuru sana mtangulizi wangu, **Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb),** na Katibu Mkuu aliyestaafu kwa heshima zote, **Dkt. Leonard Akwilapo,** kwa kazi nzuri walizofanya katika Wizara. Wameiacha Wizara pazuri na wameturahisishia kazi sana. Nampongeza sana **Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb)** kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na wenye Ulemavu.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru sana mke wangu Beatrice, watoto na familia kwa upana wake wote, ikiwa ni pamoja na mama mzazi Sekunda, kwa upendo na ukaribu ambao wamekuwa wakinipa na kunijaza nguvu na ari ya kuchapa kazi.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

**B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22**

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,519,316,801,000.00** kwa ajili ya FUNGU 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 480,474,878,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,038,841,923,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo bajeti ya maendeleo inajumuisha ongezeko la fedha za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,679,073,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha **Shilingi 1,146,780,000.00 za mishahara** na **Shilingi 1,532,293,000.00 za matumizi mengineyo**.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 540,943,008,495.63** ambapo kiasi cha **Shilingi 8,680,995,000.00** kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 532,262,013,495.63** zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2022 Wizara imekusanya **Shilingi 415,796,161,776.80** sawa na **asilimia 77** ya makadirio ambapo **Shilingi 7,622,836,164.00** zimekusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 408,173,325,612.80** zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Matumizi ya Kawaida**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2022, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 396,962,728,624.62** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na **asilimia 83** ya bajeti. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,723,003,183.30** sawa na asilimia **76** ya bajeti yake.

**Miradi ya Maendeleo**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 994,711,772,676.29** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia **96** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 684,470,232,276.01** ni fedha za ndani na **Shilingi 310,241,540,400.29** ni fedha za nje. Aidha, kiasi cha fedha za nje kinajumuisha **Shilingi 64,297,963,057.82** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19.

**C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2021/22 kwa kuzingatia vipaumbele vyake. Taarifa hiyo inapatikana ukurasa wa 19 - 69 katika kitabu cha Hotuba.

**Usimamizi wa Elimumsingi na Sekondari**

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimumsingi inatolewa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi kwa lengo la kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi na kuboresha ujifunzaji. Aidha, inaendelea kukamilisha miongozo mingine ikiwemo:

(i) Mwongozo wa Viwango na Uendeshaji wa Elimu ya Awali -*National Operational Guidelines and Minimum Standards for Pre-Primary Education* pamoja na Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo huo;

(ii) Mwongozo wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vya Shule; na

(iii) Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Shule za Msingi na Sekondari.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi, Serikali imeboresha na kutekeleza miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala; Mwongozo wa Kutoa Huduma kwa Wanafunzi katika Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala; na Mwongozo wa Wawezeshaji katika Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala. Utekelezaji wa miongozo hiyo umewezesha kurejesha shuleni wasichana 3,333 ikilinganishwa na lengo la kurejesha wasichana 3,000 walioacha shule kwa sababu mbalimbali.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Elimumsingi inatolewa kwa usawa na kuzingatia malezi bora na usalama wa mtoto shuleni, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) inaendelea na ukamilishaji wa Mwongozo wa Programu ya Shule Salama. Vilevile, imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Udahili wa Wasichana katika Shule za Sekondari;

(ii) imechapa na kusambaza Miongozo ya Kutoa Ushauri Nasaha na Unasihi nakala 44,400 ambayo itasaidia walimu kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi; na

(iii) imetoa mafunzo kuhusu huduma ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shuleni kwa walimu 243 wa shule za msingi na sekondari kutoka katika maeneo ambayo yalikuwa hayajafikiwa na mafunzo hayo.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika elimu kwa lengo la kuongeza fursa za utoaji wa elimu bora nchini. Mafanikio ya uwekezaji katika elimu ni kama ifuatavyo:

(i) usajili wa shule 741 ikilinganishwa na lengo la shule 450 zilizolengwa kama ifuatavyo; shule za awali pekee zisizo za Serikali 33, shule za awali na msingi 511 (Serikali 363 na zisizo za Serikali 148), sekondari 196 (Serikali 151 na zisizo za Serikali 45) na Chuo cha Ualimu kimoja kisicho cha Serikali; na

(ii) kuwezesha ujenzi wa shule mpya 175 (msingi 9 na sekondari 166) ambapo ujenzi wa shule 33 (msingi 9 na sekondari 24) umekamilika na ujenzi wa shule 142 za sekondari upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, imewezesha ujenzi wa madarasa 3,283, mabweni 112, ofisi 10, matundu ya vyoo 8,096, usimikaji wa vifaa vya kunawia mikono na ununuzi wa matenki ya kuhifadhia maji safi katika shule za msingi 235.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Elimumsingi nchini, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewezesha ununuzi wa magari 187 kwa ajili ya maafisa elimu msingi katika halmashauri 184 na magari matatu kwa ajili ya Baraza la Mitihani. Aidha, inaendelea na taratibu za ununuzi wa magari 185 kwa ajili ya maafisa elimu sekondari nchini.

***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imechapa na kusambaza nakala 9,903,453 za vitabu vya kiada vya masomo 14 na Kiongozi cha Mwalimu nakala 599,928 kwa Darasa la VI – VII na kuwezesha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kufikia 1:1;

(ii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada nakala 3,139,500 vya masomo ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I – V vitakavyoboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa nakala 20,422 kwa masomo 44 ya Darasa la I – VII kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu.

(iv) imechapa na kusambaza nakala 1,510,832 za vitabu vya kiada vya Kundirika la Kwanza na la Pili, Kiongozi cha Mwalimu nakala 137,500 na mihtasari nakala 16,041 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; na

(v) imekamilisha uchapaji wa nakala 6,074,000 za vitabu vya kiada aina 29 vya Sekondari Kidato cha 1 - 4 kwa masomo ya Biology, Physics, Chemistry, Mathematics, Agriculture, Home Economics, Kiswahili, Civics, Information and Computer Studies, Geography, History na English.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha huduma za maktaba nchini kwa lengo la kuamsha ari ya Watanzania kupenda kujisomea na kuelimika. Katika kufikia azma hiyo, imefanya ukaguzi na kutoa ushauri wa usimamizi na uendeshaji wa Maktaba 13 zikiwemo Maktaba ya Mkoa wa Singida, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Dodoma, Ruvuma, Mbeya, Kagera, Morogoro na Iringa pamoja na Maktaba ya Wilaya ya Mbulu na Maktaba ya Kijiji cha Mbweera iliyopo Wilaya ya Hai.

***23. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa elimu ya Msingi na Sekondari nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa mfumo wa kielektroniki (Learning Management System - LMS) wenye moduli, miongozo na vitabu mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kwa njia ya mtandao utakaotumika kutoa Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA); na

(ii) imeboresha Maktaba Mtandao ya Taasisi ya Elimu Tanzania kwa

kuiongezea uwezo wa kubeba maudhui katika miundo mbalimbali na kuongeza baadhi ya vitabu ambavyo havikuwepo. Maktaba hiyo inapatikana bure kwa anwani https://ol.tie.go.tz ambayo imerahisisha upatikanaji wa vitabu.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia upimaji na tathmini ya wanafunzi wa Elimumsingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu nchini kwa kutekeleza kazi zifuatazo:
- (i) imeendesha upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,561,599 watahiniwa kati ya watahiniwa 1,678,209 waliosajiliwa, Kidato cha Pili watahiniwa 602,955 kati ya watahiniwa 652,611 waliosajiliwa na umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 32,043 wa darasa la pili;
- (ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,108,023 kati ya watahiniwa 1,132,084 waliosajiliwa, Kidato cha Nne kwa watahiniwa 521,351 kati ya watahiniwa 538,024 waliosajiliwa. Vilevile, imeendesha Mtihani wa Maarifa (QT) kwa watahiniwa 8,324 kati ya watahiniwa 9,874 waliosajiliwa; na
- (iii) imesajili watahiniwa 88,805 wa Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) na watahiniwa 7,115 wa Mitihani ya Ualimu (Astashahada na Stashahada). Mitihani hiyo imeanza kufanyika tarehe 9 Mei, 2022.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kukusanya maoni kuhusu mitaala inayotumika katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu kutoka kwa wadau wa elimu ambapo hadi sasa jumla ya wadau 103,210 wametoa maoni. Wadau walioshiriki katika kutoa maoni ni pamoja na; Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Taasisi za kidini, Taasisi binafsi, Wataalamu mbalimbali wa elimu, na Wananchi kwa ujumla. Aidha, maoni hayo yamekusanywa Tanzania Bara na Zanzibar na yatazingatiwa wakati wa uandaaji wa mitaala mipya itakayowajengea wanafunzi ujuzi na maarifa yanayoendana na mahitaji ya jamii katika nchi, Kikanda na Kimataifa. Vilevile, mitaala hiyo itawezesha kuwaandaa wanafunzi kuendelea na ngazi ya elimu inayofuata.

**Usimamizi wa Elimu ya Ualimu**

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuongeza fursa za Elimu ya Ualimu kwa kudahili jumla ya wanafunzi 19,314 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada ambapo vyuo vya ualimu vya Serikali vilidahili wanafunzi 19,178 na visivyo vya Serikali wanafunzi 136.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu kwa kujenga upya Vyuo vitatu ambavyo ni Sumbawanga, Dakawa na Mhonda. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa Chuo kipya cha Ualimu Ngorongoro kitakachokuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 400. Aidha, imewezesha ununuzi wa kompyuta 425 ili kuboresha ufundishaji wa somo la TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha utendaji kazi kwa wakufunzi kwa kutoa mafunzo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la hisabati, sayansi na TEHAMA kwa wakufunzi 355. Aidha, imetoa mafunzo kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Vituo vya Walimu kwa walimu wawezeshaji 30,490 wakiwemo walimu wa elimu ya awali na msingi 26,657, walimu wa elimu maalum 1,882 na wawezeshaji wa MEMKWA 1,951.

**Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu inayotolewa nchini inazingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetathmini jumla ya asasi 6,524 kati ya lengo la asasi 7,263 ambazo ni: shule za Awali na Msingi 5,332; Shule za Sekondari 1,162; na Vyuo vya Ualimu 30. Aidha, imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa ushauri uliotolewa katika asasi 1,516 ikilinganishwa na lengo la asasi 1,453. Kati ya asasi hizo, Shule za Awali na Msingi 1,156, Sekondari 358, na Vyuo vya Ualimu viwili.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu Maalum**

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha uendelezaji wa elimumsingi na sekondari nchini unafanyika kwa kuzingatia usawa, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa kutekeleza yafuatayo:
- (i) imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2021/22 - 2025/26 pamoja na kuzalisha nakala kwa maandishi ya kawaida, maandishi ya nukta nundu na maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu; na
- (ii) imenunua viti mwendo 365 na vishikwambi 285 kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo na viziwi walioko katika shule za msingi na sekondari. Aidha, imenunua na kusambaza vifaa vya kielimu na saidizi 413 vikiwemo bajaji, kompyuta mpakato, vishikwambi, embosser machine na vifaa vya usikivu kwa ajili ya wanafunzi wasioona, viziwi na wenye ulemavu wa viungo katika ngazi ya Elimu ya Juu.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha elimu ya michezo na mafunzo ya skauti katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchini, kwa kutoa mafunzo kuhusu namna bora ya uendeshaji wa skauti na namna ya kukabiliana na majanga kwa walimu walezi wa skauti 100 katika Mkoa wa Mwanza, Dodoma, Manyara, Kigoma, Geita, Mara, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Katavi na Singida. Aidha, imeendesha mashindano ya michezo na sanaa (UMISAVUTA) katika Vyuo vya Ualimu.

**Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa lengo la kuongeza idadi ya wahitimu katika ngazi hiyo. Katika kufikia azma hiyo, yafuatayo yametekelezwa:
- (i) imedahili wanafunzi 266,236 katika ngazi Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada katika fani za sayansi na teknolojia shirikishi, afya na sayansi shirikishi, biashara, utalii na mipango;
- (ii) imedahili wanafunzi 90,712 kati ya lengo la wanafunzi 142,150 katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ambapo wanafunzi 428 ni wenye mahitaji maalum. Aidha, imedahili wanafunzi 15,037 katika Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi;
- (iii) imeanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma – DTC chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500;
- (iv) imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera; na
- (v) inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume - Zanzibar yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,536 ambapo ujenzi umefikia asilimia 30.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwajengea umahiri wahitimu wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo vya umahiri katika Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika Nyanja za Nishati, Usindikaji wa Ngozi, Uchukuzi na TEHAMA.

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kufanya mapitio ya mitaala na miongozo ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuhakikisha mafunzo yanayotolewa katika ngazi hiyo yanaendana na mipango ya nchi na mahitaji ya soko la ajira. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi imehakiki mitaala 51 kati ya 150 iliyoandaliwa na vyuo vya elimu ya ufundi na kutoa mafunzo ya namna ya upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 653. Aidha, imeandaa na kuhuisha mitaala 27 ya fani mbalimbali katika sekta tano ambazo ni: umeme (5), magari (8), mitambo (5), kilimo (5) na ukarimu (4).

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini inatolewa kwa vitendo kwa lengo la kukuza na kuendeleza ujuzi na umahiri. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:
- (i) imerasimisha ushirikiano na mashirika na taasisi 17 kutoka katika sekta rasmi ili kuwezesha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na walimu. Mashirika hayo ni; Shirika la Umeme Tanzania, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), TPM (1998) Ltd Morogoro, TOYOTA, Bakhresa Co. Ltd, Kilombero Sugar Co, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Tume ya Sayansi na Teknolojia, Benki ya Azania, SIDO, SFD, NSSF, NEEC, JUVE na COMPASSION; na
- (ii) imewezesha wafanyakazi 15 na wanafunzi 2,222 kwenda viwandani kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na kugharimia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 7,605 wa fani mbalimbali kwa lengo la kuwajengea ujuzi na stadi zinazohitajika.

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kwa kujengea uwezo rasilimaliwatu katika taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa kuwawezesha watumishi 31 kuhudhuria masomo katika ngazi ya Stashahada, Shahada ya Kwanza na Umahiri. Vilevile, imetoa mafunzo kwa watumishi 1,177 wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kulingana na maeneo ya ubobezi.

**Usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Elimu ya Juu inayotolewa nchini inazingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu na inaendana na mipango ya nchi, soko la ajira la Kikanda na Kimataifa, Serikali imetekeleza yafuatayo:
- (i) imewezesha tathmini ya mitaala 72 iliyowasilishwa na Vyuo vikuu nchini na kutoa ithibati kwa mitaala 31;
- (ii) imekagua na kutambua taasisi saba za nje zilizowasilisha maombi ya kuanza kupeleka wanafunzi vyuo vya nje ya nchi. Aidha, imefanya ufuatiliaji katika taasisi 14 zinazopeleka wanafunzi kusoma nje ya nchi; na
- (iii) imefanya ukaguzi katika Vyuo Vikuu 30 kwa lengo la kuhakiki ubora wa utoaji wa Elimu ya Juu. Vilevile, imetathmini na kutambua tuzo 2,111 kati ya tuzo 2,531 zilizowasilishwa ambazo zilitolewa na Vyuo vya Elimu ya Juu nje ya Nchi.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Vyuo Vikuu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:
- (i) imeratibu maombi ya wanafunzi 112,228 kati ya maombi 120,000 yaliyolengwa kwa wanafunzi kujiunga na Shahada ya Kwanza katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu 74 nchini. Kati ya maombi hayo, jumla ya waombaji 100,620 wamedahiliwa katika Vyuo Vikuu mbalimbali. Vilevile, imeratibu udahili wa waombaji 24,839 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Vyuo Vikuu ambapo jumla ya waombaji 23,110 walidahiliwa katika kozi mbalimbali;
- (ii) imeratibu ufadhili wa masomo unaotolewa na nchi rafiki kwa wanafunzi wa kitanzania 111 (Shahada ya kwanza 9, Uzamili 74, na Uzamivu 28) kama ifuatavyo: Uingereza (12), Hungaria (23), China (72), na Mauritius (4); na
- (iii) imejenga vituo vitano vya Mikoa vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika Mkoa wa Geita, Kigoma, Simiyu, Lindi na Manyara. Aidha, inaendelea na ukarabati wa Kampasi ya Zanzibar ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali imefanya maonesho ya 16 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo jumla ya taasisi 74 za ndani ya nchi zilishiriki na wadau 55,000 walihudhuria. Maonesho hayo yalitoa fursa kwa wananchi kufahamu kazi mbalimbali zinazofanywa na Taasisi za Vyuo Vikuu.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine katika uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wetu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya Kikanda na Kimataifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imehuisha Hati za Makubaliano baina ya Tanzania na nchi rafiki ambazo ni: Msumbiji, Algeria, Morocco, Zimbabwe, Poland, Umoja wa Falme za Kiarabu pamoja na Jumuiya ya Madola.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza fursa za Elimu ya Juu kwa kuboresha huduma za upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:
- (i) imetoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 569** kati ya **Shilingi bilioni 570** zilizopangwa kutolewa kwa wanafunzi 148,581. Fedha hizo zimetolewa kwa wanafunzi 177,777 kati yao wanafunzi 69,333 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 108,444 wanaoendelea na masomo. Aidha, imeboresha mwongozo wa kutoa mikopo kupitia maoni yaliyokusanywa kutoka kwa wadau; na
- (ii) imekusanya **Shilingi 156,806,093,384.02** sawa na asilimia **78** ya lengo la **Shilingi 201,319,005,000.00** zilizokadiriwa kukusanywa kutokana na mikopo iliyoiva.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:
- (i) imewezesha upanuzi wa maabara ya viumbehai katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambapo ujenzi umefikia asilimia 80;
- (ii) imeanza ujenzi wa maabara kuu ya kemia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani;
- (iii) imeboresha na kuendeleza Shamba la Mafunzo kwa kupanda miche 500 ya michikichi, malisho ya ng'ombe, kuweka uzio, kufunga mfumo wa umwagiliaji wa matone, ukarabati wa mabwawa matano ya samaki na mabwawa 12 madogo kwa ajili ya vifaranga vya Samaki katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo; na
- (iv) imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Afrika Mashariki cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia taasisi za Elimu ya Juu imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika kazi za ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali kama ifuatavyo:
- (i) imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa nyumba za Bunge eneo la Kilimani - Dodoma; majengo ya Mchapishaji Mkuu wa Serikali, Kituo cha Taifa cha Kukabiliana na Maafa – Dodoma; majengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati;
- (ii) imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu ukarabati wa majengo ya Balozi za Tanzania katika nchi za DRC, Rwanda, Oman, Saudi Arabia, Msumbiji, Malawi, Burundi na Marekani, Chuo cha Ualimu Ndala na Mpwapwa; na
- (iii) imesanifu na kusimamia vituo vya michezo katika Mkoa wa Dodoma, Geita na Dar es Salaam, Kituo cha mafunzo ya michezo 'katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya pamoja na Kituo cha Taarifa za Afya Singida.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuzingatia masuala mtambuka katika utoaji wa elimu na mafunzo nchini kwa ngazi zote kwa kutoa mafunzo kuhusu afya ya uzazi, jinsia, VVU na UKIMWI, rushwa na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa walimu 3,800 wa shule za Msingi na Sekondari, Wanachuo 1,819 wanaosoma usimamizi na uongozi wa elimu, wafanyakazi 405 na wanafunzi 3,769 wa Elimu ya Juu.

**Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko 19**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kupambana na athari za ugonjwa wa UVIKO 19 kupitia sekta ya elimu iliidhinisha afua tatu muhimu za kukabiliana na athari hizo kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19. Katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitekeleza maeneo matatu ambayo ni; Kuboresha utoaji wa elimu maalum, Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Ualimu, na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:
- (i) imeandika na kuchapa nakala 57,756 za vitabu vya Kiada, Kidato cha 1 - 4 vya maandishi yaliyokuzwa kwa masomo ya Biology, Physics, Chemistry, Mathematics, Agriculture, Home Economics,

Kiswahili, Civics, Information and Computer Studies, Geography, History na English. Aidha, imeandika, kuchapa na kusambaza vitabu vya nuktanundu nakala 9,178 kwa masomo hayo ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi 353 wasioona;

(ii) imewezesha ununuzi wa vifaa vya wanafunzi wa Elimu ya Juu wenye mahitaji maalumu katika Vyuo Vikuu 11 vya Umma kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) imewezesha ujenzi wa madarasa 41, kumbi za mihadhara tatu na mabweni 15 katika Vyuo vya Ualimu 23 vilivyonufaika na mpango huo. Ujenzi wa miundombinu hiyo utasaidia katika kupunguza msongamano wa wanafunzi;

(iv) inaendelea kuwezesha ujenzi wa vyuo vipya vya ufundi stadi vya Mikoa vinne na ununuzi wa samani katika Vyuo vya Wilaya 25 vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, inaendelea na ununuzi na usambazaji wa vifaa na mashine za kufundishia katika vyuo 34 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs); na

(v) inaendelea na ujenzi wa jengo la maabara, madarasa na ofisi katika Chuo cha Ufundi Arusha. Aidha, inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

**Usimamizi na uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa watumishi kusimamia, kuratibu na kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri 184 za Tanzania Bara kwa lengo la kuboresha uratibu wa masuala ya teknolojia na ubunifu hususan katika kuibua, kutambua na kuwaendeleza wavumbuzi na wabunifu wachanga nchini;

(ii) imewajengea uwezo watumishi 182 kati ya 300 waliolengwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kama sehemu ya maandalizi ya kupata ithibati ya viwango vya ubora vya kimataifa (International Organization for Standardization - ISO Certification); na

(iii) imewezesha jumla ya watumishi 170 wa taasisi zinazohusika na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kuhudhuria masomo ya muda mfupi na muda mrefu katika kozi mbalimbali ambapo kati yao watumishi 31 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 139 mafunzo ya muda mrefu.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa kazi za bunifu na matokeo ya tafiti yanatambuliwa Kitaifa na Kimataifa na kuendelezwa ili kuongeza kasi ya matumizi yake katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imewezesha bunifu 26 kuingia sokoni kati ya bunifu 200 zinazoendelezwa na Serikali ambazo zilipatikana katika MAKISATU ya mwaka 2019 hadi 2021. Aidha, imetambua teknolojia mpya 90 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa kufikia 479 katika kanzidata ya kitaifa.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutambua umuhimu wa kuendeleza taasisi za sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeanzisha vitalu nyumba (screen houses) vinne katika Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia vyenye ukubwa wa mita za mraba 4,900 kwa ajili ya tafiti za kilimo, kutoa mafunzo kwa vitendo, kufanya majaribio ya teknolojia zilizobuniwa na watafiti pamoja na kuzalisha mazao mbalimbali.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano Mkuu wa 65 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria mwaka 2021 ambapo Mtafiti Mtanzania **Ndugu Salum Faki Hamad** kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) alipata tuzo ya uzalishaji wa mbegu bora ya mpunga inayostahimili chumvi na magonjwa; na

(ii) imeshirikiana na mradi wa South African Innovation Support (SAIS) ili kuendeleza kazi za ubunifu nchini ambapo ushirikiano huo umeziwezesha kampuni changa mbili za Fundi *App* na *Exam Net* kushiriki katika mashindano ya *Slush 2021* yaliyofanyika Helsinki - Finland. Kupitia mashindano hayo, mshiriki mmoja **Ndugu Godfrey Gervas Kilimwomeshi** kutoka Tanzania aliibuka mshindi wa jumla na kupata zawadi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuimarisha usalama wa jamii ikiwemo kulinda afya za wafanyakazi wanaotumia teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,065 wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi kati ya wafanyakazi 1,920 waliolengwa ambapo ilibainika kuwa viwango vya mionzi vilivyopo vinakubalika kisheria; na

(ii) imepima sampuli 31,371 za vyakula, mbolea na bidhaa za tumbaku ambapo kati ya hizo vyakula kutoka nje ya nchi 9,732, vyakula vinavyosafirishwa nje ya nchi 17,864, mbolea 924, na tumbaku na bidhaa nyingine 2,851.

**Kuimarisha na Kuendeleza Tafiti na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo**

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatambua umuhimu wa utafiti katika kuleta maendeleo, kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kiuchumi na kuibua maarifa mapya. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia taasisi za elimu, mafunzo, sayansi na teknolojia imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya jumla ya tafiti 143 ikilinganishwa na lengo la tafiti 129 zilizolengwa kufanyika katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau ndani na nje ya nchi. Tafiti hizo zipo katika maeneo ya elimu, mazingira, kilimo, afya, madawa, jinsia, afya za wanyama, samaki, utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na mimea ya asili, kilimo endelevu cha mazao mbalimbali, mabadiliko ya tabianchi, misitu na rasilimalimaji;

(ii) imeendelea kugharimia tafiti na mafunzo katika Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia kupitia miradi 24 ya utafiti kwa lengo la kuzalisha wataalam na teknolojia za kisasa katika maeneo ya Kilimo, TEHAMA, Chakula na Lishe; na

(iii) imeendelea kugharimia miradi 32 ya utafiti, ubunifu na miundombinu ya utafiti inayoratibiwa kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

**D. TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara (Tume ya Taifa ya UNESCO FUNGU 18). Taarifa hiyo inapatikana ukurasa wa 70 - 72 katika kitabu cha Hotuba.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:

(i) imeshiriki katika Mkutano Mkuu wa 41 wa UNESCO uliofanyika nchini Ufaransa mwezi Novemba, 2021. Katika mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi Tendaji ya UNESCO; na

(ii) imefanikisha Lugha ya Kiswahili kuwa Lugha ya kwanza Afrika kutambuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa na kupewa siku maalum ya tarehe 7 Julai kuadhimishwa kila mwaka.

**E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba nitoe mwelekeo wa mipango na bajeti ya Wizara (FUNGU 46) katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Taarifa hiyo inapatikana ukurasa wa 72 – 108 katika kitabu cha Hotuba.

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, Kazi kubwa itakayofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 itakuwa ni kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa minajili ya kufanya maamuzi kuhusu masuala kadhaa ambayo Sera imeainisha lakini hayajatekelezwa. Kwa mfano, Sera inaainisha kwamba elimu ya lazima, yaani *compulsory education*, itakuwa ni ya miaka kumi, lakini bado tunatoa elimu ya lazima ya miaka saba. Wizara inatarajia kuwa kabla ya mwisho wa mwaka huu uchambuzi utakuwa umefanyika na kukamilika kuhusu Sera hiyo ili maamuzi yaweze kufanyika kwa utekelezaji. Pamoja na uchambuzi huo, juhudi za kukusanya maoni ya wadau zitaendelea ili maamuzi yatakapofanyika yazingatie maoni hayo na uchambuzi wa kitaaamu.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mapitio ya Sera yatatoa dira ya mabadiliko yatakayohitajika katika Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978. Hivyo, Wizara inatarajia kuwa ifikapo Desemba, 2022 itakuwa imekamilisha rasimu ya mabadiliko ya mitaala itakayozingatia maoni ya wadau na mwelekeo wa Sera ya Elimu utakaokuwa umependekezwa. Matokeo ya zoezi hilo yatawezesha uboreshaji wa elimu unaojielekeza katika elimu ya ufundi na ujuzi utakaomsaidia mhitimu kuweza kujiajiri na kuajirika.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo na mabadiliko ya mitaala ambayo Serikali inakusudia kukamilisha yataleta mageuzi makubwa ya elimu kupata kutokea hapa nchini. Wizara inatoa wito kwa wadau kuendelea kutoa maoni yao kwa sababu azma ya Serikali ni kufanya mageuzi makubwa yanayozingatia matakwa ya wananchi, kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha wahitimu kujiamini, kuajirika na kujiajiri, kuwawezesha wahitimu kumudu utandawazi, na kukidhi mahitaji ya uchumi wa nchi yetu. Kwa ujumla masuala yafuatayo yataangaliwa na kuzingatiwa:

a) Mapitio ya Sera;
b) Mapitio ya Sheria;
c) Mabadiliko ya Mitaala;
d) Idadi (mahitaji) ya Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri;
e) Ubora Stahiki wa Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri;
f) Mahitaji ya Miundombinu; na
g) Mahitaji ya Vitendeakazi.

Mambo haya saba ni budi yazingatiwe ili kuhakikisha kwamba mageuzi ya elimu tunayoyatarajia yatakuwa kweli yanakidhi mahitaji yetu.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mapitio ya sera na mabadiliko makubwa ya mitaala, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 utajielekeza katika kutekeleza maeneo ya kimkakati yafuatayo:

(i) kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi nchini;

(ii) kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini. Moja ya hatua zitakazochukuliwa ni Serikali kulipia gharama za uchapishaji na uchapaji wa riwaya bora kila mwaka itakayoandikwa na Mtanzania ili kusaidia na kuimarisha juhudi za uandishi hapa nchini;

(iii) kutekeleza juhudi za kukuza sayansi hapa nchini kwa kufanya masuala yafuatayo:

**Kwanza**, kutoa ufadhili wa asilimia mia wa kulipia gharama za masomo za Chuo Kikuu kwa wanafunzi watakaoongoza katika mitihani ya masomo ya sayansi ya Kidato cha Sita.

**Pili**, katika kutekeleza Ilani ya CCM, kutoa *scholarship* kwa Watanzania watakaofanya vizuri sana katika masomo yao ya vyuo vikuu kwenye nyanja za sayansi, teknolojia na tiba ili kwenda kusoma katika vyuo vilivyo bora zaidi duniani kama vile MIT.

**Tatu**, kuhimiza utafiti wa kisayansi na tiba katika vyuo vyetu vikuu kwa kutoa tuzo ya **Shilingi milioni hamsini** kwa mhadhiri yeyote atakayeweza kuchapisha matokeo ya utafiti wake katika majarida yenye hadhi ya juu kabisa ya sayansi na ya elimu ya tiba.

**Nne**, kuhamasisha sekta binafsi na wadau mbalimbali kufadhili Watanzania kwenda kusoma katika vyuo bora kabisa duniani. Hadi sasa, mikakati tayari imeanza kuandaliwa kwa kushirikiana na **Bwana Rupin Rajan** na wadau wengine ili kufanikisha azma hii. Kama nitakavyoeleza, tayari Benki ya NMB imekubali kutenga **Shilingi bilioni mia mbili (200)** kwa ajili ya mikopo ya Wanafunzi.

(iv) kuongeza wigo wa shule za ufundi za elimumsingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea vijana wetu stadi na maarifa yanayohitajika katika soko la ajira; na

(v) kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenye kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati utaenda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:

**a. Kuhuisha Sera, Sheria na Miongozo ya Utoaji wa Elimu Nchini**

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na mapitio ya sera na sheria, Serikali itaandaa miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) mwongozo wa usimamizi na utawala bora katika elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji katika shule za msingi na sekondari;

(iii) mwongozo wa usimamizi na ufuatiliaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kwa lengo la kuboresha mafunzo na usimamizi wa elimu katika ngazi husika; na

(iv) mwongozo wa kuanzisha, kukarabati na kuendesha maktaba kwa lengo la kuweka utaratibu unaofaa wa kuanzisha, kukarabati na kuendesha maktaba nchini.

**b. Kuendelea Kuhakikisha Watoto wote wenye Umri wa Kwenda Shule Wanapata Fursa**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenye sifa za kujiunga katika ngazi mbalimbali za elimu nchini wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa na kuhitimu. Azma hiyo, itafikiwa kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) itafanya ufuatiliaji kwa lengo la kubaini watoto wote wenye umri wa kwenda shule na kuwapa fursa ya elimu;

(ii) itaendelea kuimarisha mazingira ya ushiriki wa wadau katika utoaji wa elimu nchini; na

(iii) itaendelea kuimarisha ushiriki wa mtoto wa kike katika elimu kwa kutatua changamoto zinazomkabili ikiwa ni pamoja na ulinzi aendapo na atokapo shuleni.

**c. Kuendelea Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Awali, Elimumsingi na Sekondari, na Elimu ya Ualimu**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika ngazi ya elimu ya awali, elimumsingi, sekondari na elimu ya ualimu kwa kuendelea kutekeleza sera ya elimu bila ada katika ngazi ya elimu ya awali na elimumsingi.

**63.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuimarisha utoaji wa elimu nje ya mfumo rasmi, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (NALMERS) unaolenga kupunguza kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika. Aidha, itawezesha wasichana takribani 3,000 walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito kupata elimu kwa njia mbadala.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upimaji na tathmini ya elimumsingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendesha upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,716,776, Kidato cha Pili watahiniwa 694,336 na umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 32,363 wa darasa la pili; na

(ii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,376,169, Kidato cha Nne kwa watahiniwa 596,272 na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 8,505, Kidato cha Sita kwa watahiniwa 93,594 na Mtihani wa Astashahada na Stashahada ya Ualimu kwa watahiniwa 7,135.





**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari, na kuhamasisha tabia ya wanafunzi kupenda kujisomea vitabu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itawezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kuchapa na kusambaza nakala 2,000,000 za vitabu vya masomo ya Mathematics, *Physics, Chemistry* na *Biology.* Vilevile, itachapa na kusambaza vitabu vya kimacho na nuktanundu kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wenye uoni hafifu na wasioona.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Ufundi nchini kwa kutoa mafunzo ya elimu ya ufundi katika vyuo vya ualimu kutoka vyuo viwili vilivyopo sasa hadi kufikia vyuo saba. Vyuo hivyo vitawezeshwa vifaa, mashine, karakana na walimu wa masomo ya ufundi pamoja na kutoa mafunzo kwa wakufunzi 100 wa masomo ya ufundi katika vyuo hivyo.

**d. Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Utoaji wa Elimu Kuanzia Elimumsingi, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, na Elimu ya Juu**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha na kusogeza huduma za uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya elimumsingi, sekondari na Vyuo vya Ualimu, Serikali itajenga ofisi tano za Uthibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri ya Pangani, Ubungo, Bunda, Njombe na Tarime na kununua magari 20.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itawezesha NACTVET kufanya mapitio ya miongozo ya uandaaji wa mitaala na kutoa ithibati ya mitaala katika vituo vya umahiri vya DIT, NIT na ATC vinavyotekeleza afua za kimkakati katika ajenda ya maendeleo ambazo ni maendeleo ya TEHAMA na sekta ya ngozi, usafiri wa anga na nishati jadidifu .

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Elimu ya Juu inayotolewa nchini inazingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu, Serikali itatathmini tuzo 3,000 zilizotolewa katika Vyuo Vikuu vya nje ya nchi na kuzitambua zitakazokidhi vigezo.

**e. Kuendelea Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza fursa za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini, Serikali inatarajia kusajili vyuo 20 vya elimu ya ufundi, na vyuo 80 vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi na hivyo kuwa na jumla ya vyuo 538 vya elimu ya ufundi na vyuo 830 vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Aidha, itaendelea kusimamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Dodoma (DTC).

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha wahitimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi wanapata ujuzi na stadi za kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa, Serikali itajenga karakana sita za uchomeleaji na uungaji wa vyuma katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma vya Mkoa wa Manyara na Pwani, pamoja na karakana za umeme, bomba, magari na uashi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Kihonda.

**f. Kuendelea Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Juu**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu nchini, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaratibu udahili wa wanafunzi 133,000 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kuomba udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Umahiri. Vilevile, itaendelea kutekeleza mpango wa kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike katika programu za sayansi (Science, Technology, Engineering and Mathematics (STEM); na

(ii) itaratibu utoaji wa mikopo kwa wanafunzi 205,893 katika Taasisi za Elimu ya Juu na kufanya ukaguzi kwa waajiri 8,000 kwa lengo la kuwabaini wanufaika wapya takribani 30,000 ili kuwezesha ukusanyaji wa Shilingi 241,419,005,000.00 kutokana na mikopo iliyoiva.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya kugharimia elimu nchini kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wake ili kuendana na mahitaji yanayotokana na ongezeko kubwa la uhitaji wa mikopo. Katika kufanikisha hilo, Benki ya NMB imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 200** kwa kuanzia katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kuanza kutoa mikopo ya elimu.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Utoaji wa mikopo kutokana na fedha hizo, utasimamiwa na Benki ya NMB kwa utaratibu maalum wa kibenki. Kwa mujibu wa makubaliano kati ya Wizara na Benki, mikopo hiyo itatolewa kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(i) itatolewa kwa riba nafuu;

(ii) itatolewa kuanzia ngazi ya stashahada (Diploma) hadi ngazi ya Umahiri (Postgraduate); na

(iii) itatolewa kwa wazazi au walezi ambao ni waajiriwa wa Serikali, sekta binafsi au wafanyakazi wanaotaka kujiendeleza.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** fursa hiyo itasaidia kupunguza idadi ya waajiriwa kuomba au wazazi/walezi kuwaombea watoto wao mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na hivyo kutoa fursa kwa waombaji wenye uhitaji zaidi. Kutokana na fursa hiyo, kipekee naomba niishukuru Benki ya NMB kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za ugharamiaji wa Elimu ya Juu. Vilevile, nitambue uwepo wa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB ***Bi. Ruth Zaipuna*** ambaye tumemkaribisha katika Bunge lako tukufu. Aidha, nitoe wito kwa taasisi nyingine kuunga mkono jitihada za Serikali za kugharimia elimu nchini.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwajengea uwezo wa utendaji kazi watumishi katika taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali itaendelea kutoa ufadhili wa masomo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wanataaluma na wataalam 1,401 wakiwemo wanafunzi 65 wa kike wenye ufaulu uliojipambanua katika masomo ya sayansi.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo Vikuu, Serikali itajenga maabara 21, mabweni 19, madarasa 77, kumbi za mihadhara 13, maktaba tisa, ofisi 71, mifumo ya maji minne, vituo atamizi vitatu na studio moja. Vilevile, itakarabati mabweni 11, madarasa 50, maabara mbili, nyumba za watumishi 15 na ofisi 25 katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu. Aidha, itajenga Ndaki ya Uchumi na Mafunzo ya Biashara awamu ya pili katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Ndaki ya uchumi na mafunzo ya biashara katika Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia - Butiama.

**g. Kutegemeza Matumizi ya Sayansi na Teknolojia Katika Ufundishaji na Ujifunzaji, na Maendeleo ya Taifa**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuwaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini kwa lengo la kuendeleza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika ajenda ya maendeleo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itawaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu na wagunduzi wachanga kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuwezesha ubunifu na ugunduzi wao kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchumi. Aidha, itawaendeleza wabunifu 70 walioibuliwa kupitia MAKISATU katika mwaka wa fedha 2021/22; na

(ii) itaandaa maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wanawake na wasichana katika sayansi ili kuhamasisha ushiriki wao katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) itaendelea kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini kwa kupima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,064 wanaofanya kazi katika mazingira ya vyanzo vya mionzi. Aidha, itafanya ukaguzi katika vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyoayonisha (Non-Ionizing Radiation).

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha huduma ya teknolojia ya nyuklia nchini, Serikali kupitia TAEC itaanzisha kituo cha mafunzo ya usalama wa mionzi na nyuklia ili kuongeza wataalamu na wigo wa udhibiti wa matukio hatarishi ya kinyuklia. Aidha, itaendelea na ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza, na kuanza ujenzi wa maabara Zanzibar na katika Mkoa wa Mbeya.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaanza ujenzi wa jengo la ghorofa sita lenye vyumba vya madarasa, ofisi na maabara. Vilevile, itajenga mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam; na

(ii) itaanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 180 katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST). Vilevile, itaanza ujenzi wa jengo la utawala katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

**h. Kuimarisha na Kuendeleza Tafiti na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo**

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa taasisi za elimu, sayansi, teknolojia na ubunifu kufanya tafiti zenye tija na kutumia matokeo ya tafiti hizo katika ajenda ya maendeleo ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itawezesha kufanyika kwa tafiti 252 katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo; mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, utawala na maendeleo, mifugo, biashara na uvuvi.

**F. TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba nitoe mwelekeo wa mipango na bajeti ya Wizara (FUNGU 18) katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Taarifa hiyo inapatikana ukurasa wa 109 - 110 katika kitabu cha Hotuba.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itaendelea kuratibu na kusimamia programu na miradi mbalimbali katika nyanja za elimu, sayansi, utamaduni, habari na mawasiliano. Vilevile, itafungua ofisi ya Tume mjini Unguja - Zanzibar kwa lengo la kusogeza huduma za Tume. Vilevile, itafuatilia na kutathmini utelekezaji wa mikataba 10 ya Tume iliyoridhiwa, na kuendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani ambayo yatakuwa yakifanyika tarehe 7 Julai kila mwaka.

**G. SHUKRANI**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa jinsi tunavyofanya kazi vizuri pamoja na mchango wake katika kuandaa wasilisho hili. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Profesa Eliamani Sedoyeka na Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Mdoe na Profesa Carolyne Nombo wameongoza kwa umakini na juhudi kubwa timu ya wakurugenzi, wakuu wa taasisi na watumishi wote katika kuandaa hotuba hii. Ninawashukuru kwa dhati kwa juhudi hizi na kwa kazi kubwa wanazofanya.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi, na Wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wamiliki na Mameneja wa Shule, Vyuo na Taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu nchini.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rombo kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao. Nawaahidi utumishi uliotukuka.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Elimu wote ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Algeria, Umoja wa Falme za Kiarabu, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Malaysia, Misri, Morocco, Zimbabwe, Netherland, New Zealand, Norway, Palestina, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Benki ya Dunia, *Foreign, Commonwealth and Development Office (*FCDO), *Swedish International Development Agency* (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education* (GPE), *United Nations International Children's Emergency Fund (*UNICEF), *United Nations Development Programme* (UNDP), *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (*UNESCO), *United States Agency for International Development* (USAID), *Inter University Council for East Africa* (IUCEA), *Human Development Innovation Fund* (HDIF), *Deutscher Akademischer Austauschdienst* (DAAD), *British Council, Campaign for Female Education* (CAMFED), *Commonwealth Secretariat, Aga Khan Education Services, Japan International Cooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organization* (KTO), *Korea International Cooperation Agency* (KOICA), *Water Aid, Plan International*, *Tanzania Education Network/*Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Mo Foundation, Christian Social Services Commission (CSSC), na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

**H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23**

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,493,004,355,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

(i) **Shilingi 533,456,916,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 500,196,732,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 33,260,184,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

**91.** **Shilingi 959,547,439,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 778,083,678,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 181,463,761,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,709,163,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 1,176,870,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,532,293,000.00**).

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya **Shilingi 1,495,713,518,000.00.**

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara http://www.moe.go.tz.

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.



# Wanafunzi kutoka kaya duni wahitaji msaada

**Na Grace Mwakalinga,** MAKETE

SERIKALI na wadau wa elimu wameombwa kuwasaidia watoto zaidi ya 400 kutoka familia duni katika kata za Matamba, Kimani na Mlondwe wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe ambao wanakosa masomo kutokana na ukosefu wa mahitaji ya shule na baadhi yao kuwa watoro.

Ombi hilo limetolewa jana na wadau wa elimu wilayani Makete wakati wakikabidhi msaada wa vifaa vya shule kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye kipato duni katika kata za Matamba, Kimani na Mlondwe wilayani humo.

Wadau hao, akiwamo Claudy Mahenge, walitoa vifaa mbalimbali vya shule vyenye thamani ya Sh. milioni 10 ikiwamo sare za shule, madaftari, taulo za kike pamoja na vifaa vya vya kufundishia na kujifunzia.

Mahenge alisema waliamua kutoa msaada huo baada ya kuona watoto wengi wanakatisha ndoto zao kwa sababu ya kukosa mahitaji muhimu ya shule.

"Mimi ni mkazi wa Makete, hivyo vikwazo vyovyote vinavyowakabili wanafunzi vinanigusa moja kwa moja, dunia imebadiliki hatuwezi kuona watoto wetu wanaishi mazingira magumu ambayo nasi tuliyapitia, tuna kazi ya kufanya kuhakikisha tunajitoa kwa hali na mali ili watoto wetu wasome kwenye mazingira mazuri na kutimiza ndoto zao," alisema Mahenge.

Akizungumzia msaada huo ambao ni mwaka wa sita sasa kutolewa kupitia Taasisi ya Maria Foundation ya jijini Mbeya, mwakilishi wa taasisi hiyo, Haroun Muhavile, alisema lengo ni kuhakikisha watoto wanasoma kwenye mazingira rafiki.

Alisema wadau mbalimbali wenye asili ya Makete ambao wanaishi maeneo mbalimbali nchini, walikubaliana kukusanya fedha ili kuwasaidia watoto wenye mahitaji hususani wanaosoma shule za msingi na sekondari.

Mratibu wa misaada inatolewa na taasisi hiyo kwa wanafunzi wilayani Makete, Mwalimu Yohana Nyenye alisema zaidi ya watoto 1,000 wamenufaika na misaada hiyo na kwamba wengi wao wako elimu ya juu.



Mratibu wa Shirika la Jhpiego kwa Mkoa wa Mbeya, Waziri Njau (kushoto), akitoa mafunzo kwa wauguzi namna ya kutoa huduma rafiki kwa vijana, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC aagiza maboresho miundombinu Nanenane

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAANDALIZI ya maonyesho ya wakulima (Nanenane) kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yameanza kufanyika jijini Mbeya huku kukiwa na tatizo la uchakavu wa baadhi ya miundombinu uliosababishwa na maonyesho hayo kutofanyika mwaka jana kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19.

Kikao cha kwanza na maandalizi ya Nanenane Nyanda za Juu Kusini kilifanyika juzi na kuwahusisha wakuu wa mikoa, wataalamu wa idara ya kilimo na mifugo pamoja na wakulima kutoka mikoa saba ya Nyanda za Juu Kusini.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema hali ya miundombinu ya viwanja vya Nanenane (John Mwangale) siyo nzuri na kuagiza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuboresha barabara zote za ndani ya viwanja hivyo kabla ya mwezi Agosti mwaka huu.

"Hiki ni kikao chetu cha kwanza lakini miongoni mwa mambo tunayopaswa kuyashughulikia kwa haraka ni kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya viwanja hivi vya Nanenane maarufu kama John Mwakangale, naawagiza TARURA kushughulikia jambo hilo mapema kabla ya mambo hayajaanza kupamba moto huku mbeleni kwa sababu kuna mambo mengi ya kuyatekeleza kwenye maadhimisho hayo," alisema Homera.

Akizungumzia hali ya uwanja wa maonyesho hayo, Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Donard Bombo, alisema miongoni mwa sababu zilizochangia miundombinu ya uwanja huo kuharibika ni kutofanyika kwa maonyesho hayo mwaka jana kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 ambao unaisumbua dunia.

Alisema kwa vile hali ya ugonjwa huo ni shwari kulinganisha na ilivyokuwa awali, wamejipanga kuboresha miundombinu yote muhimu ndani na nje ya uwanja huo ili kufanikisha maadhimisho ya maonyesho ya wakulima ambayo kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yatafanyika jijini Mbeya katika viwanja vya John Mwakangale.

Baadhi ya wakuu wa mikoa walioshikiri kikao hicho akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, walisema hatua ya serikali kurejesha maonyesho hayo ni fursa nzuri kwa wakulima kujifunza mbinu bora za kilimo na kutaka umakini uwapo katika matumizi ya fedha za maandalizi ya maonyesho hayo.

## Walia gharama usafiri wa bajaj

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BAADHI ya abiria wanaotumia usafiri wa bajaj jijini Mbeya wameendelea kuiangukia serikali kupunguza bei ya usafiri huo kwa madai wanashindwa kuimudu kutokana na hali ngumu ya maisha.

Uamuzi wa kupandisha nauli uliotangazwa hivi karibuni na uongozi wa madereva bajaj Jiji la Mbeya na kuanza kutekelezwa Jumatatu ya wiki iliyopita.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya abiria walidai gharama za maisha zimekuwa kubwa, hivyo wanaiomba serikali kukaa meza moja kujadiliana na uongozi wa bajaj kupanga bei rafiki ambayo itaendana na hali ya uchumi kwa sasa.

"Mimi nashangaa nimempa dereva Sh. 1,000, cha ajabu ananirudishia chenji ya Sh. 200, nilipomhoji ndio akaniambia kuwa nauli imepanda halafu mimi nilikuwa nategemea hiyo hela iniwezeshe kurudi nilipotoka kwa maana kwamba nauli ni Sh. 500. Nimelazimika kutembea kwa mguu kutoka Mwanjelwa hadi Mzumbe," alilalamika Tumaini Mwaipopo, mkazi wa Sabasaba.

Tumaini alishauri ni vyema wangepandisha nauli angalau ifikie Sh. 600 kuliko kuweka 800 kwa kuwa gharama hizo zinaongeza makali ya maisha kwa wananchi hususani wakati huu ambao Taifa linapitia kwenye mfumuko wa bei za bidhaa.

Sara Aliko, mkazi wa Sinde ambaye ni mchuuzi wa samaki, alisema kupanda kwa gharama za nauli ya bajaj kutaathiri biashara yake kwa kuwa kila siku lazima anunue kwa bei ya jumla kwenye soko la Soweto na kila anapokwenda na kurudi anatumia usafiri wa bajaj.

Sara anahofia kuwa kutokana na mzunguko wake wa kila siku, kuna hatari kutopata faida kutokana na kuwa atalazimika kuchukua Sh. 400 kila siku kama fidia ya kiwango cha nauli kilichopanda kwa safari ya kwenda na kurudi.

Fodingo Allen, dereva wa bajaj, alisema abiria wengi hawafahamu gharama mpya za nauli, hivyo wanaendelea kuwaelekeza lakini hawaachi kuwabeba wale wenye nauli ya zamani.

"Sisi tulitaka iwe Sh. 1,000 kabisa kwa sababu kutokana na gharama za vifaa na mafuta, tunajikuta hela tunayoingiza kwa siku haikidhi mahitaji na malengo yetu ya siku," alisema.

Mwenyekiti wa wamiliki na madereva wa bajaj Jiji la Mbeya, Festo Mwasimba, alisema wameamua kupandisha nauli kutokana na kupanda kwa bei za vipuli na vifaa vya bajaj.

Alisema nauli ya awali ilikuwa Sh. 500 na imedumu kwa takribani miaka tisa na kwamba kiwango hicho hakiendani na mahitaji pamoja na uendeshaji wa vyombo hivyo katika kipindi hiki.



# Wanawake wataka uwakilishi Maulamaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wanawake wameomba kuwapo kwa uwakilishi wa kundi kwenye Baraza la Maulamaa, ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili, ikiwamo ya kusikilizwa matatizo yao ya ndoa na talaka.

Hayo yalisemwa jana na Mwakilishi wa Konde, Zawadi Amour Khamis, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia makadirio, mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema katika muundo wa Baraza la Maulamaa Zanzibar, hakuna uwakilishi wa wanawake, na kwamba kwa bahati mbaya masuala yanayowahusu kundi hilo hakuna wa kuyajadili kwa kina.

Aidha, alisema ni muhimu kwa ofisi ya Mufti mkuu kuwapo kwa kitengo kitakachoshughulikia changamoto za wanawake, ikiwamo masuala ya ndoa ambayo ni muhimu yakashughulikiwa na kusuluhishwa na wanawake wenyewe kuliko kusikilizwa na wanaume.

"Mwaka jana nilipochangia muswada wa kuanzishwa kwa ofisi ya Mufti nilizungumzia suala la wanawake kuingizwa katika Baraza la Maulamaa, lakini ilishindikana ingawa nimeulizia kwa mashekhe mbalimbali ambao wanasema siyo dhambi wanawake kuwamo katika baraza hilo," alisema.

Naye Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema wanawake wanahitaji nafasi hizo katika baraza hilo ili changamoto zinazowakabili zitatuliwe na maulamaa wanawake.

Alisema hatua kubwa imepigwa kimaendeleo na kwamba wapo wanawake wenye elimu ya kutosha kuingia kwenye taasisi hizo ili kutoa mchango wao kwenye mambo yahusuyo dini.

"Upo umuhimu mkubwa kwa wanawake kuingizwa katika Baraza la Maulamaa hatua itakayosaidia kuyajadili mambo yanayowahusu moja kwa moja, ikiwamo migogoro ya ndoa na talaka," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Viti Maalumu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdalla, alisema amefurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na ofisi ya Mufti kwa kutoa elimu ya mafunzo kwa wanandoa kabla ya kuingia makubaliano ya kudumu ya ndoa ambayo yamepunguza utoaji wa talaka kiholela.

## Bilioni 3/- zawezesha wajasiriamali 4,000

**Na Mwandishi wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetumia zaidi ya Sh. bilioni tatu kuwawezesha wajasiriamali 4,173 kukuza kipato chao, kupitia wakala wa uwezeshaji wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi, Abdalla Abassi Wadi, ndani ya Baraza la Wawakilishi aliyetaka kujua lini wakala huyo ataanza utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema mfuko huo umeanza kazi rasmi baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kutia saini uanzishwaji wake unaolenga kushughulikia wajasiriamali wadogo katika matumizi ya fedha zilizotengwa kwa makundi hayo.

Alieleza kuwa vikundi vilivyopata fedha kwa upande wa Unguja ni wajasiriamali 1,878 na Pemba ni vikundi 2,295, na kwamba fedha zitatolewa na benki ya CRDB, iliyopewa jukumu la kusimamia utoaji wa fedha hizo.

Aidha, alisema serikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 36 kwa ajili ya wajasiriamali wadogo kutekeleza majukumu yao ya uwekezaji katika miradi mbalimbali ya kiuchumi.

Alisema serikali kupitia wakala wa uwezeshaji kiuchumi imetenga fedha zingine Sh. bilioni 35 kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wa mazao ya baharini, ikiwamo mwani, majongoo ya baharini pamoja na ufugaji wa samaki na kaa.



Baadhi ya wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama, wakifuatilia kikao cha bajeti cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Serikali yafafanua lengo kituo marekebisho kitabia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema kuwa lengo la serikali kuanzisha kituo cha tiba na marekebisho ya tabia ni kuwarudisha waraibu (watumiaji wa dawa za kulevya) katika hali ya kawaida.

Aliyasema hayo jana wakati alipofanya ziara katika kituo cha tiba na marekebisho ya tabia huko Kidimni Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Hemed alisema waraibu waliopo kituoni huko ni rasilimali inayotegemewa kwa ujenzi wa taifa na familia, hivyo ni jukumu la serikali kuhakikisha huduma bora zinapatikana kwa vijana waliopo katika kituo hicho na vituo vingine.

Makamu wa Pili ambaye ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, ameupongeza uongozi wa mamlaka hiyo kwa kuanzisha miradi ya maendeleo pamoja na kuwapatia ujuzi ambao utawasaidia pindi watakapoacha utumiaji wa dawa hizo na watakapo toka kituoni huko na kurudi katika jamii zao.

Aliutaka uongozi huo kununua mashine ya kutotoleshea vifaranga ili kumaliza changamoto ya upatikanaji wa kuku pamoja na kuhakikisha ng'ombe wanapatikana, ili kuboresha utoaji wa huduma kwa vijana waliopo kituoni hapo jambo ambalo litawasaidia kufikia malengo ya kituo hicho.

Pia, aliupongeza uongozi wa mamlaka hiyo kwa uamuzi wao wa kupunguza gharama za miradi hatua ambayo itasaidia fedha hizo kutumika katika maeneo mengine.

Akiwasalimia waraibu waliokuwapo kituoni hapo, aliwataka kuwa watiifu na nidhamu ili lengo la kuwepo kituoni hapo kufikiwa na taifa lipate vijana watakaolitumikia kwa kuleta maendeleo.

Kamishna wa Mamlaka hiyo, Kanal Burhani Zuberi Nasoro alieleza kuwa kituo kilianzishwa Januari 2022 na kina waraibu 34 na lengo kuu ni kubadilisha tabia ya waraibu hao kurudi katika mazingira ya kawaida.

Kanal Burhani alieleza kuwa kituo hicho kina miradi ya majengo ya ofisi pamoja na miradi ya ujasiriamali ikiwamo ufugaji wa ng'ombe na kuku, ushoni, kilimo cha mboga pamoja na eneo la ufundi wa gari (karakana).

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA MADAI NA. 27/2020**
**SADALLAH IBRAHIM SADALLAH ......................MDAI**
**DHIDI YA**

- **NEMGANGA SADALLAH**
- **ISAYA MPANGALA............WAJIBU MAOMBI**

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma, Mbele ya Mhe. A. S. KAGOMBA, Jaji wa Mahakama Kuu Tanzania Dodoma, saa nne (4:00) kamili asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 16/05/2022.

**HIVYO BASI;** Mnatakiwa mfike ninyi wenyewe au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** hamtofika ninyi wenyewe au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo ninyi au wakili wenu kuwepo.

**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 mwezi wa May,2022.





**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.61/ 2022**
**In the matter of the estate of the late HONORATI LUDOVICK RITE of KINYAMBWA within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LEVINA PASCHAL RITTE.**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 6, 2022

**Date at Dodoma this 19TH Day of APRIL, 2022**




## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOB WASADA MLIGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari(MITSUBISHI) yenye namba za usajili **T149 CHN** Chassis namba: **JTFDP626400033205** Injini namba : **4D34139893** Chasis Namba: **TYAFE659FGDS1795** Kadi Namba : **5510507** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MKB/TR/RB/93/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ELIAH WANJARA NYEOJA AMEPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA T 580 DWU AINA YA TOYOTA PREMIO SALOON CHASSIS NAMBA: ZZT2450003904 ENGINE NAMBA: 1ZZ0986449 **TAARIFA YA POLISI: MZN/RB/4238/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BERNARD CHARLES OKAMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 954 BKP** aina ya **TOYOTA CRESTA GF GX100 SALOON** rangi ya silver yenye CHASSIS NAMBA **GX1006169910** na ENGINE NAMBA **1G6828149** TAARIFA YA POLISI: **MZN/RB/4238/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI.

**ABDUNI ABSWAI HAMISI** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki aina ya **TOYO** yenye namba za usajili **T 747 ARF.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0754389125.** Polisi taarifa **MAS/RB/TR/06/2022.**

## TANGAZO LA MNADA

Work ethic company limited Kwa idhini tuliyopewa na FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Nyumba na viwanja katika maeneo tofauti katika jiji la Dar es salaam ,Wateja wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Conjestar Lawrence Kaugala | Kiwanja chenye je ngo kipo chanika | 25.05.2022 |
| Imelda Adam Lyanzile | Nyumba ipo kifuru | 26.05.2022 |
| Frola Honest Mosha | Nyumba ipo luguluni Ubungo | 27.05.2022 |
| Prosper Faustin Tarimo | Nyumbo ipo Ngoma mapindunzi kigamboni | 28.05.2022 |
| Regnat January Kassian | Nyumba ipo kichangani kigamboni | 28.05.2022 |
| Benjamini Matiko Chacha | Nyumba ipo kigamboni Mkwajuni | 28.05.2022 |
| Ally Nassoro Kimbugu | Nyumba ipo Temeke kwa Nyoka | 29.05.2022 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315 (Workethic) au 0623662447 (Workethic) au 0677014355(Fanikiwa)**

***Uza, Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa***

***Bei Poa Tupigie***

***0782253676***

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Mtoto wa Museveni mahakamani akidaiwa kuutaka urais Uganda

**KAMPALA, Uganda**

MAHAKAMA ya kikatiba ya Uganda, imemtaka mtoto wa Rais Yoweri Museveni, Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba, kujibu shtaka analotuhumiwa la kueleza nia yake ya kuwania nafasi ya urais akiwa bado anahudumu ndani ya jeshi.

Kulingana na tovuti ya Daily Monitor imeripoti kuwa wakili wa haki za binadamu Gawaya Tegulle aliiomba mahakama hiyo iliyoitishwa katika mji mkuu, Kampala, kumzuia Jenerali Kainerugaba kufanya shughuli za kisiasa akiwa bado anatumikia jeshi.

Gawaya pia anataka jenerali huyo afunguliwe mashtaka ya uhaini kufuatia madai yake ya njama ya kumrithi baba yake kwa kutumia mbinu haramu.

Jenerali Kainerugaba, kamanda wa jeshi la nchi kavu la Uganda, ana siku 10 kuwasilisha majibu yake.

Mnamo tarehe 2 Mei, alitangaza mipango ya kuzindua mpango wa kisiasa, na kuchochea uvumi kwamba alinuia kumrithi baba yake kwa muda mrefu.

Mnamo Machi 8, alitangaza kustaafu kutoka kwa jeshi kwenye Twitter lakini Rais Museveni alikataa kumuandaa mwanawe kuchukua wadhifa wake.

**BBC**

## Usafirishaji wahamiaji Rwanda kucheleweshwa

**LONDON, Uingereza**

MPANGO wa kupeleka baadhi ya wahamiaji wanaotafuta hifadhi nchini Rwanda uliotaka kufanywa na serikali ya Uingereza utachukua muda kuanza kutekelezwa.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Uingereza, Priti Patel, alisema mpango huo unahusisha watu wanaotafuta hifadhi baada ya kuonekana kuwa wameingia nchini Uingereza kinyume cha sheria.

Katika utaratibu huo, watu hao watasafirishwa hadi nchini Rwanda wakati maombi yao yanashughulikiwa.

Alisema mpango wa kupeleka baadhi ya watu kuomba hifadhi katika nchi hiyo ya Afrika Mashariki utatoa ishara ya wazi kwamba hakutakuwa na haki ya kusalia Uingereza.

Waziri hiyo alisema, wizara yake itaanza kuwafahamisha watu kwamba watahamishwa hadi Rwanda hivi karibuni, lakini ilikiri kwamba ucheleweshaji ulitarajiwa kutokana na changamoto za kisheria.

Aliongeza kuwa serikali imejitolea kutekeleza mpango huo na itatumia kila chombo na kila sheria iliyo nayo kumwondoa yeyote anayefika nchini humo kinyume cha sheria".

Alipoulizwa kama ana uhakika mpango huo utafanya kazi na utachukua muda gani kuanza, Patel alisema: "Nimesema tangu siku ya kwanza, hata niliposaini mkataba na kutangaza ushirikiano, kwamba hii itachukua muda na itachukua muda kwa sababu mbalimbali."

**BBC**

# Marekani yapitisha sheria kukopa vifaa ulinzi kuibana kivita Russia

**WASHNGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani Joe Biden, ametia saini Sheria ya Kukodisha kwa Mkopo vifaa vya ulinzi ili kurahisisha utaratibu wa kusambaza silaha nchini Ukraine.

Kipengele hicho kilichopewa jina la "Sheria ya Kukodisha ya Kulinda Demokrasia nchini Ukraine ya 2022," iliwasilishwa katika Bunge la Congress hata kabla ya kuanza kwa uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Mei 3, mswada huo uliidhinishwa kwa kura nyingi za Baraza la Wawakilishi la Bunge la Marekani, wabunge 417 waliunga mkono, huku 10 walipinga.

Kwa mujibu wa muswada huo, Rais wa Marekani anaweza kuidhinisha serikali kukopesha au kukodisha mali ya ulinzi kwa Ukraine au nchi nyingine za Ulaya Mashariki zilizoathiriwa na uvamizi wa Russia ili kusaidia kuimarisha ulinzi wa nchi hizo na kulinda raia dhidi ya mashambulizi yanayoweza kutokea au kuendelea, uchokozi kutoka upande wa Russia.

Muswada huu utafanya kazi sawa na sheria ya kukodisha ya Vita vya Kidunia vya pili, wakati Marekani iliwapa washirika wake silaha, vifaa vya kijeshi na chakula bila malipo ya mapema na kwa kuchelewa kwa muda mrefu.

Wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, mmoja wa wapokeaji wakuu wa misaada kama hiyo alikuwa Umoja wa Kisovieti.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alishukuru Marekani na Biden kwa kufufua mpango wa msaada.

"Asante POTUS na watu wa Marekani kwa kuunga mkono Ukraine katika kupigania uhuru na mustakabali wetu," akaunti rasmi ya Rais wa Ukraine ilituma ujumbe huo kupitia Twitter kwa lugha ya Kiingereza.

Makombora yashambulia kituo cha biashara

Russia imeshambulia kwa makombora kituo cha biashara mjini Odesa na kusababisha hasara kubwa.

Katika picha zilizochapishwa mtandaoni na jeshi la Ukraine, wazima moto wanaonekana wakikanyaga vifusi vya kile kilichokuwa kituo cha biashara na ghala.

Moshi mnene na mweusi ulisambaa katika mji huo wa bandari lakini kwasababu ya amri ya kutotoka nje mitaa ilikuwa tupu wakati makombora yalipopigwa usiku.

Mamlaka inasema mtu mmoja alifariki na wengine watano kupelekwa hospitalini.

Mashambulizi hayo yalitokea juzi jioni, siku hiyo hiyo ambayo rais wa Baraza la Ulaya alikuwa katika mji huo.

Charles Michel alisema aliona maghala yaliyojaa nafaka, ngano na mahindi huko Odesa ambayo yalikuwa tayari kusafirishwa nje ya nchi lakini yamezuiwa.

Tishio la usalama wa chakula duniani ni jambo lililosisitizwa na Rais Zelensky wa Ukraine katika hotuba yake ya usiku.

Alisema kuwa bila Ukraine kusafirisha nje, nchi kadhaa ..."walikuwa tayari wana uhaba wa chakula na kwamba hali inaweza kuwa ya kutisha".

***BBC***



Rais wa Ukraine, Vladimir Zelensky (wapili kushoto), akimwangalia mbwa aliyepewa jina la Pattern baada ya kumtunuku tuzo ya heshima ya Rais kwa huduma zake tangu uvamizi wa Russia. **PICHA: BBC**

# Goodluck Jonathan akataa uteuzi wa APC

**ABUJA, Nigeria**

RAIS wa zamani wa Nigeria, Goodluck Jonathan, amekataa kupokea fomu ya uteuzi wa urais kupitia chama tawala cha APC.

Chama cha All Progressives Congress (APC) kilimtoa madarakani Jonathan 2015 baada ya kuwa kwenye nafasi hiyo kwa miaka mitano.

Kundi la wafuasi lilinunua fomu ya uteuzi kwa niaba yake siku ya Jumatatu, mtindo ambao hutumiwa na wawaniaji wengi kununua fomu hiyo kupitia wandani wao.

Lakini taarifa iliyotolewa na msemaji wa rais huyo wa zamani, ilisema Jonathan hakuwa na ufahamu wa hatua hiyo na hakuidhinisha.

"Tunasema kwamba ikiwa rais wa zamani alitaka kugombea uchaguzi, angeweka wazi nia yake kwa umma na wala sio kutumia mlango wa nyuma," ilisema taarifa hiyo.

Vyama vikuu vya kisiasa nchini Nigeria vinatarajiwa kufanya uteuzi baadaye mwezi huu ili kufikia mwisho wa kupata majina yawagombea iliyowekwa na tume ya uchaguzi Juni 3.

Fomu inachukua gharimu karibu dola 240,000 au paundi 5,000 kununua fumu za ya uteuzi wa APC.

Yeyote atakayepata uteuzi kutoka Chama cha APC wa uchaguzi atakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Chama cha PDP.

***BBC***

HABARI MICHEZO

# MAYELE MBONA WAKAWAIDA SANA - BEKI TANZANIA PRISONS

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuhakikisha mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, anashindwa kufurukuta na kupasua ukuta wa Tanzania Prisons, beki wa kati wa timu hiyo ya 'Wajelajela', Vedastus Mwihambi, ameibuka na kudai straika huyo ni mchezaji wa kawaida sana.

Timu hizo zilikutana juzi katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na kumalizika kwa sare tasa, huku Mayele mbali ya kunyimwa fursa ya kuziona nyavu, lakini alishindwa kukwamisha penalti nyavuni baada ya kuachia shuti kali lililopaa juu ya lango.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwihambi alisema Kocha wao Mkuu, Patrick Odhiambo, alimpa mbinu madhubuti za kumkaba Mayele asiweze kuwafunga, ambazo alizifanyika kazi ipasavyo na kufanikiwa kutimiza jukumu alilopewa.

"Mwalimu alituambia tutakapokutana na Yanga, tumkabe Mayele mpaka mwisho ili bila kumpa nafasi, jambo ambalo tumefuata maelekezo na kupata matokeo ya sare," alisema Mwihambi.

Alisema anashukuru wamepata matokeo hayo kwani wameweka rekodi ya kutofungwa na timu ambayo inaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC.

Mwihambi alisema lengo ni kupambana akishirikiana na wachezaji wenzake wapate pointi tatu kwenye kila mchezo ambao upo mbele yao ili wajinusuru kushuka daraja.

"Lengo ni kuipambania timu yetu iendelee kushiriki Ligi Kuu ya NBC, licha ya kuwa na ushindani mkubwa kwa sasa," alisema.

Licha ya kushindwa kuziona nyavu katika mchezo huo, bado Mayele anaendelea kuwa kileleni mwa wafungaji bora msimu akiwa sambamba na George Mpole wa Geita Gold FC kila mmoja akiziona nyavu mara 12.

Kwa matokeo hayo sasa Yanga imefikisha pointi 57 kileleni zikitokana na mechi 23, wakati Tanzania Prisons yenyewe ikiwa na alama 23 katika nafasi ya 14.



Baadhi ya waogeleaji wa klabu ya FK Blue Marlins wakiwa katika picha ya pamoja. **MPIGAPICHA WETU**

# Mashindano ya kuoegelea kufanyika Dar Jumamosi

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Kuogelea ya FK Blue Marlins yamepangwa kufanyika Jumamosi na Jumapili kwenye Bwawa la Shule ya Kimataifa ya FK iliyopo Bahari Beach, Dar es Salaam.

Meneja wa Klabu ya FK Blue Marlins, Opalina Nanyaro amesema mashindano hayo yatashirikisha waogeleaji kutoka klabu mbalimbali ambapo kila klabu imepewa nafasi ya waogeleaji 30.

Opalia alisema maandalizi ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na waogeleaji wanafanya mazoezi ili kushindania zawadi mbalimbali siku hiyo.

Alisema wanatarajia waogeleaji zaidi ya 200 kushiriki katika mashindano hayo yaliyodhaminiwa na Shoppers, Kahawa Cafe, Cool Blue, EFM, Doctors Plaza Polyclinic, PRO Fixers Tanzania, FK International Schools, Viscar Integrated Consulting (TZ) Limited na Coca Cola, GardaWorld. Kwa mujibu wa Opalina waogeleaji watashindana katika umri tofauti na staili mbalimbali kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Alisema mbali ya staili tano za kuogelea, waogeleaji hao watashindana katika 'relei' ambayo kwa mtindo wa Individual Medley (IM) na Freestyle. Kwenye IM, lakini watachanganya staili nne ambazo ni butterfly, backstroke, breaststroke, na freestyle.

"Waogeleaji watakaoshinda katika mashindano hayo watazawadiwa medali na vikombe, tunawaomba wadhamini wajitokeze ili kufanikisha mashindano haya ambayo ni maarufu na yenye mvuto mkubwa," alisema Opalina.

## Droo 8-bora Soka la Ufukweni kesho

**Na Saada Akida**

HATUA ya nane bora ya Ligi ya Soka la Ufukweni mkoa wa Dar es Salaam, inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Mei 20, mwaka huu katika viwanja vya Ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam.

Ligi hiyo ambayo ilikuwa na makundi mawili, katika Kundi A, timu zilizosonga mbele ni Friends of Mkwajuni, Ilala FC, Savannah Boys na Vingunguti Kwanza wakati Kundi B zikiwa ni Kisa FC, Kijitonyama Sand Heroes, Msasani Mabingwa na Mburahati FC.

Kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawasa, baada ya kukamilika kwa hatua ya makundi, sasa ligi hiyo inaenda kuchezwa hatua ya nane bora na droo itafanyika kesho, Alhamisi katika ofisi za Shirikisho la Soka Tanzania, TFF.

"Droo itafanyika TFF kila timu itamjua mpinzani wake atakayecheza naye katika hatua ya nane bora ili kutafuta bingwa wa ligi hiyo kwa msimu wa 2022," alisema Pawassa.

Wakati huo huo, Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema usajili wa dirisha dogo kwa klabu za soka la ufukweni umefunguliwa tangu jana hadi Juni 16, mwaka huu.

"Klabu zinatakiwa kukamilisha usajili na uhamisho wa wachezaji kwa wakati, na kama kuna changamoto yoyote, klabu zinatakiwa kuwasiliana na Idara ya Mashindano ya TFF kwa sababu hatutakuwa na muda wa ziada wa kufungwa kwa dirisha," alisema Ndimbo.

## Coastal yajigamba Biashara haitoki leo

**Na Cheji Bakari, Tanga**

BAADA ya kuibuka na ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, Coastal Union imetamba kuendeleza wimbi la ushindi itakapoikaribisha Biashara United kutoka mkoani Mara katika mchezo wa mzunguko wa 23 wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini hapa leo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa na Mashabiki wa Coastal Union, Salim Bawazir ametamba kuwa lazima wawafunge Biashara United kama walivyowafunga Polisi Tanzania FC.

"Hawa Biashara United ni wakwetu tu, lazima tuibuke na ushindi kama tulivyofanya kwa Polisi Tanzania FC, hawachomoki," alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Coastal Union ipo nafasi ya 12 ikiwa na jumla ya alama 24 sawa na KMC iliyopo nafasi ya 24 ikiwa nafasi ya 11 ikipishana tofauti ya alama moja na Biashara United yenye pointi 23 ikiwa nafasi ya 13 baada ya timu hizo kila moja kucheza michezo 22.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**STERLING ATAKIWA ARSENAL**

ARSENAL wanaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, kama Manchester City itakubali kumuuza mwishoni mwa msimu huu, ambapo mkataba wake utakuwa umebaki mwaka mmoja. ***(Telegraph)***

**MANE KUTUA BAYERN**

KLABU ya Bayern Munich inapanga kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, huku magwiji hao wa Ujerumani wakiwa tayari wamewasiliana na wakala wa mchezaji huyo. ***(Sky Germany via Metro)***

**CHAMBERLAIN HAJUI HATIMA**

NYOTA wa Liverpool, Alex Oxlade-Chamberlain mwenye umri wa miaka 28, anahofu na mustakabali wake pale Anfield, ambapo hajaambiwa lolote kuhusu mkataba mpya na hajacheza mchezo wowote tangu Machi 20, mwaka huu. Mkataba wa kiungo huyo unamalizika msimu ujao. ***(Mail)***

**POGBA AIKATAA CITY**

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake na Manchester United unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ameiambia Manchester City kwamba hana nia ya kujiunga nayo akielezwa kwamba nyota huyo ataelekea klabu nyingine tofauti. ***(Athletic, via Mirror)***

**ELNENY NA MKATABA MPYA**

ARSENAL pia wameanza mazungumzo na kiungo wake Mmisri Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Athletic)***

**TUCHEL KUUNGWA MKONO**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel anatarajiwa kuelezwa kwamba ataungwa mkono na wamiliki wapya wa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

**10 KUUZWA NEWCASTLE**

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe, atasikiliza ofa za wachezaji karibu 10 katika dirisha lijalo la usajili akiwamo nahodha, Jamaal Lascelles mwenye umri wa miaka 28, huku mlinzi huyo akikosa namba kwenye kikosi hicho. ***(Sun)***

**SALTER ASAKWA LEEDS**

MLINZI wa Chelsea, Jake Clarke-Salter mwenye umri wa miaka 24, anasakwa na Leeds United na PSV Eindhoven baada ya kuonYesha kiwango bora akiwa kwa mkopo na Klabu ya Championship, Coventry City. Nyota huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, anakaribia kumaliza mkataba wake Stamford Bridge. ***(Sun)***

**XAVI AFUNGUKA BARCA**

KOCHA wa Barcelona, Xavi amesema hali yao kifedha inawaondoa katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland, ambaye anajiandaa kutua Manchester City kutoka Borussia Dortmund. ***(ESPN)***

**ADEYEM HUYOOO DORTMUND**

MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg na Ujerumani, Karim Adeyem mwenye umri wa miaka 20, anakaribia kutua Borussia Dortmund baada ya Manchester United kushindwa kumsajili, amesema wakala wake. ***(Metro)***

**BELLINGHAM ANUKIA SUNDERLAND**

KLABU ya Sunderland inataka kumsajili Jobe Bellingham ambaye ni mdogo wa kiungo wa Borussia Dortmund na England, Jude.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KUTHIBITISHWA RASMI MAN CITY WIKI HII

●●●Takriban sehemu zote za uhamisho huo zimekubaliwa na kilichobaki sasa ni...

**MANCHESTER, England**

UHAMISHO wa Erling Haaland kutoka Borussia Dortmund kwenda Manchester City unaweza kuthibitishwa wiki hii.

Kwa mujibu wa BBC Sport, uhamisho wa pauni milioni 63 wa mshambuliaji huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 21, umekubaliwa.

Inaaminika kwamba, takriban sehemu zote za uhamisho huo zimekubaliwa, huku City wakihitaji tu kuanzisha kifungu cha kukamilisha uhamisho huo.

Uhamisho huo utakuwa moja ya usajili mkubwa zaidi wa kipindi cha majira ya joto.

Wakala wa wachezaji, Mino Raiola alikuwa amehusika katika majadiliano kabla ya kifo chake, na washirika wake wakichukua hatua zaidi.

Ingawa City wapo kwenye nafasi ya kutwaa taji la Ligi Kuu England kwa mara ya pili mfululizo bila mshambuliaji wa kati, kocha Pep Guardiola amekuwa akisisitiza kuwa na nia ya kuwa na straika mmoja.

City walijaribu sana kumpata Harry Kane kutoka Tottenham msimu uliopita, lakini Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy alikataa kumuuza.

Hata hivyo, wakati Kane akiwa amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake, Haaland ni mpango rahisi kuhitimisha kutokana na kifungu chake cha kuachiwa.

Amefunga mabao 92 ya ligi katika mechi 121 akiwa na Molde, Red Bull Salzburg na Dortmund.

Mwaka jana alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufikisha mabao 20 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,255

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
KAGERA SUGAR
1 | 1.26
X | 4.69
2 | 10.74

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: GERRARD ANAWEZA KURITHI MIKOBA YANGU



**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amebainisha kuwa mchezaji wa zamani wa klabu ya hiyo, Steven Gerrard anaweza kurithi mikoba yake miaka ya baadaye.

Klopp mwenye miaka 54, hivi karibuni amesaini mkataba mpya na klabu hiyo ambao utamuweka kwenye dimba la Anfield hadi mwaka 2026.

Hiyo itamfanya kuwa kocha wa kwanza kuiongoza klabu hiyo kwa miaka 10, tangu Tom Watson afanye hivyo.

Awali, Klopp alisema kuwa ataachana na klabu hiyo baada ya muda wake kuisha.

Klopp alipoulizwa uwezekano wa Gerrard kurithi mikoba yake kwenye dimba la Anfield alisema, "Anaweza kuwa mrithi wangu? Ndio, bila shaka, inawezekana. Sina wazo lolote. Kwa hiyo nadhani inawezekana, hivyo ndivyo ilivyo."

Liverpool kwa sasa wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu nyuma ya Man City ambao wanaongoza ligi kwa alama tatu zaidi, na jana Jumanne walikuwa wakicheza dhidi ya Aston Villa.

Klopp kwenye kipindi chake tangu atue dimba la Anfield amefanikiwa kubeba ubingwa wa Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Carabao.

Huku akiwa na mchezo wa fainali ya FA dhidi ya Chelsea na mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi yaa Real Madrid msimu huu.

# Brazil vs Argentina kurudiwa

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), limetupilia mbali rufaa ya Brazil na Argentina ya kutotaka kurudia kucheza mchezo wa kufuzu wa Kombe la Dunia na sasa mchezo huo utarudiwa.

Mchezo huo ambao ulisimama dakika chache baada ya kuanza pale moja wa Ofisa wa Afya wa Brazil alipoingia uwanjani na kumzuia mmoja wa mchezaji wa Argentina anayecheza Ligi Kuu England kutokucheza kwa madai kuwa amevunja kanuni za ugonjwa wa corona.

Timu zote zimefuzu kushiriki Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka huu, huku Brazil ikiongoza kundi na Argentina ikifuata kwa kushika nafasi ya pili.

"Baada ya kuchambua malalamiko ya pande zote na kufuatilia jambo lililotokea kwenye kesi hii, kamati ya rufani imethibitisha kwamba mchezo utarudiwa," ulisema waraka wa FIFA.

FIFA awali walitoza faini ya dola 50,322 kwa vyama vyote viwili vya mpira vya Brazil na Argentina kwa sababu ya kuahirishwa kwa mchezo huo. Pia waliwapiga faini nyingine ya kutosimamia vizuri suala la usalama kiasi cha dola 250,000.



5,316,060

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/05/22 | 20:00 | Niort vs Valenciennes | 2.42 | 3.18 | 2.83 |
| 02. 14/05/22 | 20:00 | Nancy vs PAU FC | 2.34 | 3.27 | 2.88 |
| 03. 14/05/22 | 20:00 | Nimes vs Bastia | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 04. 14/05/22 | 22:00 | Bordeaux vs Lorient | 2.29 | 3.49 | 2.84 |
| 05. 14/05/22 | 22:00 | Toronto FC vs Orlando City | 2.45 | 3.44 | 2.78 |
| 06. 14/05/22 | 22:30 | Colorado Rapids vs Los Angeles FC | 2.39 | 3.57 | 2.77 |
| 07. 15/05/22 | 13:30 | Bologna vs Sassuolo | 2.58 | 3.47 | 2.48 |
| 08. 15/05/22 | 16:00 | Leeds vs Brighton | 2.34 | 3.33 | 2.83 |
| 09. 15/05/22 | 16:00 | Watford vs Leicester | 2.77 | 3.52 | 2.30 |
| 10. 15/05/22 | 16:30 | St. Pauli vs Fortuna Dusseldorf | 2.28 | 3.56 | 2.77 |
| 11. 15/05/22 | 16:30 | Sandhausen vs Holstein Kiel | 2.62 | 3.47 | 2.44 |
| 12. 15/05/22 | 18:30 | Degerfors vs Helsingborg | 2.44 | 3.22 | 2.63 |
| 13. 15/05/22 | 19:30 | Villarreal vs Real Sociedad | 2.31 | 3.56 | 2.80 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 11/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5434 | Polisi Tanzania vs Dodoma FC | 2.22 | 2.67 | 3.64 |
| 16:00 | 1089 | Coastal Union vs Biashara United | 2.47 | 2.62 | 3.20 |
| 16:30 | 2928 | Cagliari Youth vs Juventus Youth | 3.07 | 3.65 | 2.00 |
| 17:00 | 5914 | Al Masry Club vs Ghazl EL Mahallah | 2.33 | 2.73 | 3.58 |
| 18:30 | 2340 | PAOK vs Aris Salonica | 1.92 | 3.17 | 4.17 |
| 19:00 | 1525 | Randers vs Aalborg | 2.24 | 3.40 | 3.00 |
| 19:00 | 3423 | Sonderjyske vs Nordsjalland | 2.98 | 3.48 | 2.21 |
| 19:00 | 3528 | Simba vs Kagera Sugar | 1.26 | 4.69 | 10.74 |
| 19:30 | 2812 | AEK Athens vs PAS Giannina | 1.35 | 4.56 | 8.73 |
| 19:30 | 4272 | Argesul Pitesti vs Voluntari | 2.18 | 2.88 | 3.41 |
| 19:30 | 4861 | El Ittihad Alexandria vs Smouha Club | 2.74 | 2.74 | 2.89 |
| 20:00 | 2295 | Hradec Kralove vs Viktoria Plzen | 5.66 | 4.15 | 1.56 |
| 20:00 | 2862 | Banik Ostrava vs Slavia Prague | 6.86 | 4.64 | 1.43 |
| 20:00 | 3894 | Nice vs St Etienne | 1.51 | 4.28 | 5.57 |
| 20:00 | 3995 | Osasuna vs Getafe | 2.60 | 2.90 | 2.95 |
| 20:00 | 4360 | Molde vs Odd Ballklubb | 1.40 | 4.96 | 6.34 |
| 20:00 | 5148 | AIK Football vs Malmo | 2.39 | 3.01 | 2.86 |
| 20:00 | 5799 | Sparta Prague vs Slovacko | 1.67 | 3.99 | 4.75 |
| 20:00 | 5811 | Alaves vs Espanyol | 2.11 | 3.35 | 3.35 |
| 20:30 | 3721 | Sivasspor vs Alanyaspor | 2.14 | 3.26 | 3.07 |
| 21:00 | 1234 | Olympiakos vs Panathinaikos | 1.92 | 3.13 | 4.27 |
| 21:00 | 1426 | PSV Eindhoven vs NEC Nijmegen | 1.15 | 7.36 | 12.93 |
| 21:00 | 2691 | Copenhagen vs Silkeborg | 1.76 | 3.83 | 4.08 |
| 21:00 | 3782 | Utrecht vs AZ Alkmaar | 2.98 | 3.57 | 2.15 |
| 21:00 | 4230 | GO Ahead Eagles vs Feyenoord | 5.94 | 4.75 | 1.43 |
| 21:00 | 4270 | Ajax vs Heerenveen | 1.13 | 8.13 | 13.88 |
| 21:00 | 4590 | Waalwick vs Heracles Almelo | 2.24 | 3.36 | 2.97 |
| 21:00 | 5260 | Cambuur vs Willem II Tilburg | 2.52 | 3.50 | 2.52 |
| 21:00 | 5268 | Sparta Rotterdam vs PEC Zwolle | 2.34 | 3.27 | 2.88 |
| 21:00 | 5624 | Twente vs Groningen | 1.58 | 3.97 | 5.16 |
| 21:00 | 5905 | Fortuna Sittard vs Vitesse Arnhem | 2.58 | 3.47 | 2.48 |
| 21:30 | 1282 | Brugge vs Union Saint Gilloise | 2.19 | 3.39 | 3.10 |
| 21:30 | 1290 | Dundee Utd vs Celtic | 13.94 | 6.57 | 1.17 |
| 21:30 | 3520 | Leeds vs Chelsea | 4.64 | 4.05 | 1.62 |
| 21:30 | 4338 | Servette Geneva vs FC Lugano | 2.23 | 3.38 | 3.03 |
| 21:30 | 4446 | Sevilla FC vs Mallorca | 1.60 | 3.81 | 5.42 |
| 21:30 | 4841 | FC Sion vs FC Luzern | 2.39 | 3.59 | 2.65 |
| 21:45 | 2407 | Rangers vs Ross County | 1.21 | 6.39 | 10.99 |
| 21:45 | 2451 | St Mirren vs Livingston | 2.47 | 3.03 | 2.93 |
| 21:45 | 2478 | Monchengladbach vs Ukraine | 3.06 | 3.25 | 2.15 |
| 21:45 | 2552 | Leicester vs Norwich City | 1.41 | 4.65 | 6.33 |
| 21:45 | 3136 | Watford vs Everton | 4.07 | 3.57 | 1.81 |
| 21:45 | 3240 | St Johnstone vs Aberdeen | 3.32 | 2.93 | 2.31 |
| 21:45 | 3612 | Stockport vs Torquay | 1.46 | 4.16 | 6.34 |
| 21:45 | 5232 | Motherwell vs Hearts | 2.93 | 3.32 | 2.31 |
| 22:00 | 1245 | Juventus vs Inter | 3.19 | 3.24 | 2.21 |
| 22:00 | 2791 | Misr Lel Makasa vs Pyramids | 6.58 | 3.94 | 1.49 |
| 22:00 | 4845 | Nantes vs Rennes | 4.99 | 4.29 | 1.56 |
| 22:15 | 2892 | Wolverhampton vs Manchester City | 9.97 | 5.08 | 1.28 |
| 22:30 | 2440 | Elche vs Atletico Madrid | 5.39 | 3.70 | 1.63 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SPORTPESA YAIKABIDHI SIMBA MIL. 50/- KWA MAFANIKIO CAF

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Burudani na Michezo ya SportPesa imeikabidhi Klabu ya Simba hundi ya shilingi milioni 50 ikiwa ni bonasi yao kutokana na mafanikio iliyoyapata kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kutinga hatua ya robo fainali.

Hafla hiyo ya makabidhiano ilifanyika kwenye Ofisi za SportPesa, Masaki jijini Dar es Salaam jana ikihudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni hiyo, Tarimba Abbas na Meneja Uhusiano na Mawasiliano Sabrina Msuya, huku kutoka Simba ikiwakilishwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez, Meneja Miradi, Belinda Paul, Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally pamoja na mwakilishi wa wachezaji wa klabu hiyo, Erasto Nyoni.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Tarimba alianza kwa kuwapongeza wachezaji na viongozi wa Simba kwa hatua waliyofikia hii akieleza hiyo inaonyesha ni jinsi gani timu pamoja na uongozi wake wamedhamiria kufika mbali.

"Napenda kuwapongeza viongozi na wachezaji wa Simba SC kwa hatua na mafanikio ambayo mmeyapata, kwani mmewapa heshima kubwa Wanamsimbazi kote nchini. Kubwa zaidi ni heshima mliyotupa sisi wadhamini wenu wakuu kwa namna mlivyoweza kuliwakilisha taifa na kupambana mpaka kufikia hatua hii.

"Hii ni ishara nzuri kwani tuna matumaini kwenye mashindano yajayo mtashiriki kwa kujipanga vizuri zaidi na kufika hatua za mbele zaidi ya mlipofikia, ili kutimiza lengo lenu kama timu," alisema Tarimba.

Aliendelea kwa kufafanua kuhusu kiasi hicho cha pesa ambacho kimetolewa na wadhamini wakuu wa Simba, SportPesa kuwa klabu hiyo imeitendea haki nembo yao.

"Simba imeitendea haki nembo yetu SportPesa na kampuni inaamini sisi kama wadhamini wakuu imekuwa ni moja ya chachu iliyosababisha Simba Sports Club kufuzu hatua hii.

"Tunachokifanya leo ni kutimiza moja ya ahadi tuliyotoa wakati tunasaini mkataba wa udhamini mwaka 2017 kuwa tutatoa bonasi ya shilingi milioni 50 endapo mojawapo ya timu tunazozidhamini itafuzu katika hatua ya robo fainali kwenye Kombe la Shirikisho ama Ligi ya Mabingwa Afrika."

Kwa upande wa Simba, Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara alianza kwa kusema: "Nichukue nafasi hii kupongeza SportPesa kwa kufuata kila makubaliano yaliyopo kwenye mkataba kwa kutoa bonasi ya shilingi milioni 50 baada ya kufanikiwa kufika robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Sportpesa imekuwa ikitoa bonasi kila tunapofanya vizuri katika michuano mbalimbali iwe ya ndani au ya kimataifa na hilo ni kwa mujibu wa mkataba, nawapongeza sana.

"Tunaamini Sportpesa wamekuwa chachu kubwa kwetu kufanya vizuri katika michuano mbalimbali kutokana na motisha wanayotoa tena kwa wakati.

"Katika kipindi chote cha mkataba wetu mmekuwa mkitimiza makubaliano kutokana na mafanikio tuliyopata, tunaamini mna mchango mkubwa."

SportPesa ni wadhamini wakuu wa klabu ya Simba na Yanga kwa kipindi cha miaka mitano sasa.

# Tiketi Kombe la Dunia zaisha TFF

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limetangaza kusitisha maombi ya uuzaji wa tiketi za Fainali za Kombe la Dunia zinatakazofanyika Oktoba mwaka huu nchini Qatar, baada ya kutimiza idadi ya waombaji waliotakiwa.

Kwa mujibu wa tangazo lao lililolewa jana nchini kupitia mtandao wa Instagram wa TFF, imewataka wale ambao wanahitaji kwa sasa kuomba kupitia moja kwa moja kwenye mtandao wa Shirikisho la Soka Duniani, FIFA.

"Tumesitisha kupokea maombi ya tiketi za Kombe la Dunia baada ya waombaji kufikia idadi iliyotengwa. Kwa wale ambao bado wanahitaji tiketi, waombe moja kwa moja kupitia mtandao wa FIFA." TFF iliandika kwenye mtandao wake jana.

Idadi hiyo ya maombi ya tiketi imetimia kabla ya muda uliowekwa, kwani taarifa ya TFF iliyotolewa Mei Mosi na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wake, Cliford Ndimbo, ilisema inapokea maombi kwa watu wote wanaotaka tiketi kutuma maombi hadi Mei 12, mwaka huu.

Michuano hiyo ambayo itafanyika kwa mara ya kwanza barani Asia, itaanza kutimua vumbi nchini Qatar kuanzia Novemba 21 na kumalizika Desemba 18, ikizishirikisha jumla ya timu 32, ikiyashirikisha mabara sita ambayo yataumana kulisaka kombe hilo ambalo kwa sasa linashikiliwa na Ufaransa ambayo ililitwaa mwaka 2018 nchini Urusi.

**HAPA MWISHO...**




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akipiga hesabu za kumtoka beki wa Tanzania Prisons, Vedastus Mwihambi, ambaye alimnyima nafasi ya kucheka na nyavu kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi baada ya kumdhibiti vilivyo wakati timu hizo zikitoka suluhu juzi. HABARI UK. 20. **MPIGAPICHA WETU**

Michezo

Jumatano Mei 11, 2022

Nipashe



## Haaland kuthibitishwa Man City wiki hii

BONASI YA CAF...




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Sportpesa, Tarimba Abbas (wa pili kushoto), na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Sabrina Msuya (kushoto), pamoja Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez na beki wa klabu hiyo, Erasto Nyoni, wakionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 50 baada ya kukabidhiwa jana na SportPesa ikiwa ni bonasi ya kufuzu robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika. Kulia ni Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally. HABARI UK. 23. **PICHA SPORTPESA**

# WAKALA AIACHIA SIMBA KUAMUA HATIMA PABLO

●●●Huku akipania kuifumua Kagera Sugar leo bila Morrison, Chama, asema bado ana mkataba lakini....

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakishuka dimbani leo kuikaribisha Kagera Sugar kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuanzia saa 1:00 usiku, Wakala wa Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya soka nchini, Pablo Franco, Mkenya Edgar Mitema, ameanika hatima yake ndani ya kikosi hicho.

Simba ipo nafasi ya pili ikiwa na alama 46, watashuka dimbani kusaka pointi tatu muhimu ili kuzidi kujiweka katika mbio za ubingwa na kupunguza wigo wa alama kutoka kwa vinara wa ligi hiyo, Yanga yenye pointi 57 kileleni, lakini ikiwa mbele kwa mchezo mmoja.

Kikosi cha Simba kitashuka dimbani kikiwakosa wachezaji wake wanne ambao ni majeruhi, lakini watatu kati yao wakiwa wameanza mazoezi ya viungo chini ya uangalizi wa madaktari.

Nyota hao ni Clatous Chama, Chris Mugalu na Bernard Morrison ambao walikosekana katika mchezo uliopita dhidi ya Ruvu Shooting uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1. Pia itamkosa kiungo mkabaji Jonas Mkude ambaye aliumia katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting.

Kuelekea mchezo huo wa leo, Pablo amesema maandalizi yanaendelea vizuri na itakuwa mechi ya ushindani mkubwa, lakini matarajio yake ni kufanya vizuri licha ya kutambua kwamba Kagera Sugar ni timu nzuri na mechi ya awali Simba ilipoteza.

"Tumejiandaa vizuri, mashabiki wajitokeze kwa wingi kusapoti timu yao, tumejipanga kusaka ushindi katika mchezo wetu wa kesho (leo), licha ya kutokuwapo kwa baadhi ya wachezaji hao, kutakuwa na mabadiliko madogo na watakaopata nafasi watapambana kutafuta matokeo mazuri ya ushindi," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

Kocha Msaidizi wa Kagera Sugar, Buberwa Bilikesi, alisema: "Tumejiandaa vizuri na tunaingia uwanjani kuweka rekodi yetu vizuri, kuhakikisha tunaenda kupambana kutafuta pointi muhimu katika mchezo huu dhidi ya Simba."

Katika hatua nyingine, Wakala wa Kocha Mkuu wa Simba, Pablo, Mkenya Edgar Mitema amesema hatima ya mteja wake iko mikononi mwa viongozi wa klabu hiyo.

Akizungumza kutoka nchini Kenya, Mitema alisema kocha huyo anatakiwa na klabu nyingi kwa sasa, na si Orlando Pirates ya Afrika Kusini pekee bali hata Horoya ya Guinea ni miongoni mwa zinazohitaji huduma yake, lakini bado ana mkataba wa mwaka mmoja na Klabu ya Simba, hivyo ili klabu zinazomhitaji zimpate, ni lazima maamuzi yatoke kwa viongozi hao.

Wakati Mitema akisema hayo, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu amesema kwa sasa hawawezi kusema lolote mpaka hapo ligi itakapomalizika, pamoja na Kombe la FA na baada ya hapo watakaa chini na kuangalia mafanikio yalipopatikana kwanza.

"Kulikuwa na ofa ya Orlando Pirates kabla hata ya droo ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, kulikuwa na ofa nyingine Horoya, lakini ana mkataba wa mwaka mmoja na Simba, hivyo ni lazima tuheshimu mkataba. Ofa ziko nyingi, lakini tutaangalia mwishoni kama Simba inataka kumbakisha au la, hilo tutajadiliana mwishoni mwa msimu," alisema wakala huyo raia wa Kenya.

## Nabi amtetea Mayele penalti

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikitoka sare ya tatu mfululizo juzi huku akimtetea Fiston Mayele kwa kukosa penalti, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema katika mbio za ubingwa hawatakiwi kuangalia mpinzani wao bali wanaelekeza nguvu katika kupambana tu.

Nabi aliyasema hayo juzi usiku baada ya kukamilika kwa dakika 90 dhidi ya Prisons na timu hizo kutoka suluhu katika mchezo huo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nabi alisema matokeo yao dhidi ya Tanzania Prisons hayakuwa mazuri kutokana na kupoteza pointi mbili kuelekea mbio za ubingwa na sasa anaangalia namna ya kuweka mambo sawa timu kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao.

Alisema kuhusu tofauti ya pointi 11 na aliyekuwa chini yake (Simba), kwenye mbio za ubingwa hawezi kumfikiria mpinzani wake, kwani anachotakiwa kuangalia yeye na wachezaji wake ni mapungufu ya kikosi chako ikiwa ni pamoja na mashabiki kushirikiana kurejesha morali kwa wachezaji ili kuendelea na mapambano.

"Suala la ubingwa siwezi kulizungumzia kwa sababu ninachoangalia ni nini nifanye ili kurudisha morali ya wachezaji wangu kwa lengo la kwenda kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Nabi.

Kuhusu Mayele, Nabi alisema:"Hakulazimisha kupiga penalti ili awe mfungaji bora bali alipiga kwa ajili ya kutafuta ushindi, mechi ilikuwa na ushindani na wachezaji walipambana, lakini matokeo si mazuri."

Alisema mbali na kukosa penalti hiyo pia walitengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia na kwamba hilo ameliona na wanarejea mazoezini kufanyia kazi kwa ajili ya michezo ijayo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >